# *Imani Ndiyo Hisi Ya Sita*

. . . inatukomboa na kutuokoa na hisi zetu tano tulizowekwa ndani yake, hapo mwanzo. Na hiyo hisi ya tano chini . . . Yoyote ya hizo hisi tano, mwanadamu alianguka pale pamoja na hizo hisi kwa hamu yake ya chakula.

2 Sasa, tambua ya kwamba hisi hizi ulipewa upate tu kuwasiliana na makazi yako ya duniani, upate kuona, kuonja, kugusa, kunusa na kusikia, lakini kamwe hazipaswi kukuongoza. Na sasa mara nyingi . . .

3 Vipi kama nikikataa kuangalia tena, nami niyafunge tu macho yangu, na kusema, "Nakataa kutazama." Vema, macho yangu hayawezi kunitumikia tena. Vema basi, mimi, hatimaye nitakuwa kipofu. Ndipo basi mvulana wangu atakapokuja, nitayafunga macho yake kabisa, na kusema "La, bwana, hakuna kitu kama kuona." Nitayafunga tu macho yake, nimzuie kuona.

4 Akasema, "Baba yangu aliniambia hakuna kitu kama kuona, kwa hiyo nitayafunga macho ya mvulana wangu." Vema, muda si muda mwajua, kizazi chetu kingezaliwa kipofu. Hiyo ni kweli. Usipotumia hisi zako sita, zinakuwa zimelala, hazitafanya kazi hata kidogo.

5 Ndugu, hivyo ndivyo kanisa limeifanyia hisi ya sita Mungu aliyomweka ndani yake. Aliweka tu imani kando katika miujiza na ishara, na vitu vinavyowasiliana na Mungu, vinavyompa Roho Mtakatifu, na kadhalika, ameviweka hivyo *kule*, ama *huko* nyuma mahali fulani, mpaka kitu hicho kimekufa. Hiyo ni kweli. Hajui jinsi ya kuitumia, kitu hicho ni bure tu kwake.

Unasema, "Vema, Mungu ni Mponyaji."

"Loo, vipi kuhusu hilo? 'Mungu ni Mponyaji.'"

6 Kama aliwahi kuwa Mponyaji, Yeye angali ni Mponyaji; kama aliwahi kuwa Mwokozi, Yeye angali ni Mwokozi; kama aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Kwa hiyo, mnaona, ni ukosefu wa imani ambao umehubiriwa watu, unaowafanya kuacha hiyo hisi ya sita, ambayo ni imani, ikae bwete. Na mwaka mzima watakimbia nje, wawe wagonjwa, na kukimbia kwa daktari na kusema, "Daktari, loo, nina shida fulani."

7 Daktari aiangalie, aseme atajaribu. Mtu huyo, daktari mzuri, mwaminifu atafanya kazi kwa subira awezavyo, kwa nguvu zote ambazo Mungu atampa kufanya kazi na kufanya mambo ambayo anapaswa kufanya kukusaidia. Ndipo muda si muda wajua, unaenea, vema anasema, "Inanibidi tu kukwambia, hakuna cha zaidi niwezacho kufanya. Ukitaka kwenda kwa daktari mwingine, nenda ukamwone."

8 Vema basi, unamwendea daktari mwingine, yeye anasema, "La, hakuna kitu kinachoweza kufanywa, umeenea sana."

9 Sasa, huo ndio wakati, huo ndio wakati wa kuita hisi ya sita. Huo ndio wakati wa kumkubali Mungu. Huo ndio wakati wa kumtegemea Roho wa imani ambaye Mungu ameweka ndani yako.

10 Na sasa, wakati watu wamefundishwa dhidi yake kwa muda mrefu sana, inalifanya gumu. Ndugu Boze alikuwa akiniambia leo, akasema, "Ndugu Branham, kamwe sikutambua kile ulichokabiliana nacho." Mnaona? Hatambui ni kitu gani, ni kitu kigumu jinsi gani, utakapoleta, na nguvu za Mungu zitashuka moja kwa moja akiwa *halisi* sana kwa watu, wanaweza kuangalia na kuona Roho akitenda kazi miongoni mwa watu na kufanya mambo, na wengine wataketi pale, waseme, "Loo, kama ungeweza tu kufanya *hivi*, ama kufanya *hivi*, ama kufanya *vile*, ama *chochote kile*, labda ingenisaidia."

11 Loo, ndugu, kama hiyo hisi ya sita ingeweza kuelewa kile ambacho tumekuwa tukihubiri juma hili, amina, kwamba Roho Mtakatifu, Mungu alitoa ahadi hii, Kristo alitoa ahadi! Tumelipitia kwenye Maandiko juma hili, huku na huku, na huku na huku, na kulichambua, mpaka *tunajua* ya kwamba Mungu aliahidi kufanya jambo hili analofanya sasa katika siku hii, la kimbinguni.

12 Sasa, imani halisi ya kweli ingeona jambo hilo na kulishika, na pepo wote kutoka kuzimu kamwe wasingeweza kumtikisa atoke kwake. Lakini tunajikwaa kwake; haitumiki vya kutosha. Tunategemea sana zile tano. Na wakati mwingi sana, kwa asilimia tisini na tano ya watu ama zaidi, mara wanapoona zile hisi tano zimekwisha, "Vema, yote yamekwisha, chimbeni kaburi langu, andaeni jeneza langu." Mnaona?

13 Loo, nilikuwa nikiwazia juu ya maskini mwanamke mmoja hapa niliyekuwa naye kwenye mahojiano siku moja ama mbili zilizopita, siwaoni hapa sasa, jina la huyo mtu ni, kwa namna fulani ni Kije-. . . *Dorch*, *Dach*, ama . . . Dauch. Naye mke wake, aliota ndoto, ndipo akaja akiniambia ndoto hiyo, naye akasema, "Ndugu Branham, ni—niliota kwamba ibilisi alikuja kando ya kitanda changu. Naye akaniangalia na kuanza kunionyesha nyuso za tabasamu, za kuchekesha, na kusema, 'Nimekupata sasa!'"

14 Kisha kasema, "Mimi, jambo fulani tu likanipata, ndipo nikaruka kutoka kitandani na kusema, 'Ondoka hapa ibilisi, katika Jina la Yesu!' Ndipo nikaanza kumfukuza, naye akakimbia na kutoka nje ya nyumba." Naye akasema, "Sielewi hilo linamaanisha nini." Ndipo Roho Mtakatifu, akiwapo, akatoa tafsiri.

15 Muda mfupi tu baada ya hapo, mumewe akashikwa na mshtuko wa moyo. Ndipo alipomwona mumewe akianguka, naye

ni mtu mkongwe, mtu mzito, na mikono yake ikarudi nyuma, na macho yake yametokeza. Mauti yakaja kumchukua, bali Mungu hakuwa amemalizana naye, imani ya maskini mwanamke huyo iliinuka na kusema, "Sitavumilia hilo! Ninayaita maisha yake, katika Jina la Yesu Kristo!" Akapona. Mnaona?

16 Kwa nini? Hiyo hisi ya sita iliinuka katika wakati huo muhimu sana, wakati huo ulikuwa umempa imani. Mungu alikuwa amempa hiyo ndoto, ingawa haikuwa imetafsiriwa kwake bado. Lakini nikasema, "Hiyo hapo tafsiri yako."

17 Ndipo maskini huyo jamaa akaanza tu kupiga mayowe na kumsifu Mungu, akasema, "Hivyo hasa ndivyo ilivyotukia." Mnaona? Hiyo ni . . . Sasa, hiyo inaingia katika neema. Mnaona? Akampa hiyo ndoto, bila hata kujua ilikuwa ni nini, bali Mungu ni mwenye shukrani na mwaminifu, kwa vyovyote vile, kuwafahamisha watu wake.

18 Laiti tungekuwa tu wa kiroho na kutumia hiyo hisi ya sita, sisi, loo, ni mambo mangapi tungeweza kuyakwepa, ni mambo mangapi tungejua kama Kanisa lilikuwa katika utaratibu, ambapo roho na karama za Kanisa zingekuwa zikifanya kazi, tungekuwa na kina Anania na kina Safira wamelazwa pande zote, kila mahali. Hiyo ni kweli. Dhambi ingekuwa nje ya Kanisa.

19 Lakini tunakuwa wa kidunia sana kwa hisi zetu, hata tu, "Vema, kama siwezi kuliona, kama siwezi . . ." Halafu hizo hisi, ibilisi anaingia katika hisi hizo, naye atakuruhusu kuona kitu fulani kwa macho yako, na halafu ukose kuliamini, kwa vyovyote vile. Kwa sababu mara nyingi umeyafunga macho yako kwa muda mrefu sana mpaka wewe ni kipofu.

20 Jamaa fulani aliniambia wakati mmoja, kasema, "Nipofushe, nipofushe! Kama unaamini katika uponyaji wa Kiungu, Roho Mtakatifu yeye yule ambaye Paulo alihubiri, nipofushe."

21 Nikasema, "Siwezi kulifanya, kwa sababu wewe tayari ni kipofu." Nikasema, "Baba yako ibilisi alifanya hivyo muda mrefu uliopita." Mnaona? "Wewe—wewe—wewe—wewe—wewe ni kipofu tayari." Kwa kuwa Biblia ilisema yeye ni kipofu.

22 Injili hii ni, kama imefichwa kwa mtu yeyote, ni wale walio vipofu, ambao hawajajaribu kutumia hisi zao. Hisi ya, Mungu aliwapa. Hisi hiyo, kama ikitumiwa, ni hisi ya ukombozi wakati hizo zingine tano zinaposhindwa.

23 Kwa hisi hii kumekuwa na mambo makuu yaliyofanywa. Hapa wakati fulani uliopita katika mmoja wa mikutano yangu kulikuwako na mama mmoja aliyepitia jukwaani, naye alikuwa na tumbo lenye vidonda, akitokwa na damu. Ndipo Roho Mtakatifu akaanza kunena, ambalo alijua nisingeweza kufanya hivyo, na kumwambia yeye alikuwa ni nani, alikotoka, alikuwa na tumbo lenye vidonda. Ndipo alipomaliza akasema, "BWANA ASEMA HIVI, umeponywa." Naye akaenda nyumbani.

24 Tena kulikuwa na mama mmoja...ujirani alikuwa huko chini kabisa kwenye mstari wa maombi, lilipokuja, alikuwa na uvimbe kooni mwake, basi wakati mstari wa maombi ulipomfikia, akamwambia, kasema, akamwambia yeye ni nani, alikotoka, yote kuhusu hilo. Akasema, "Hilo ni sawa."

Kasema, "BWANA ASEMA HIVI, umeponywa."

25 Na kwa hiyo, hao wanawake wawili wakaenda usiku huo, wakakutana, hawakujisikia tofauti yoyote.

26 Hilo halina uhusiano wowote nalo. Hilo halina uhusiano hata mmoja nalo, kama unajisikia. Wewe—wewe huninii... Ziondokee hisia hizi, kama utazitegemea huwezi kuitegemea *ile*. Kwa sababu ni bayana ya vitu usivyoviona, kuonja, kugusa, kunusa, wala kusikia. Unaona? Ni hisi nyingine.

27 Angalieni kilichotukia: Yapata majuma mawili yakapita. Mwanamke huyu aliyekuwa na tumbo lenye vidonda, alijaribu kula, naye karibu afe, lakini angali alishikilia, akasema, "Kuna kitu cha kimbinguni kulihusu, kwa sababu huyo mtu hajawahi kuniona maishani mwake, na hata hivyo, aliniambia mimi ni nani. Nalo halina budi kuwa ni la kiungu, kwa sababu linalingana na Biblia." Mnaona? Ndipo akasema, "Nami ninamjua jamaa huyo, ninamsikia akihubiri naye hana elimu, hajui lolote kuhusu mambo haya, na aliniambia yote kuyahusu, na mtu yuyo huyo alisema, 'BWANA ASEMA HIVI.' Na kama yeye ni mtumishi wa Mungu, asingeweza kusema hilo kama tu aliliwazia, ni Roho Mtakatifu akinena kupitia kwake kwamba, 'Umeponywa.'" Naye akaendelea.

28 Naye mu—mume wake alikuwa Mkristo, watoto wake. Ndipo akasema...Naye angeenda kumwona maskini rafiki yake wa kike huko chini mtaani kutoka kwake aliyekuwa na lile fundo, hakuna tofauti. Lakini wote wawili walikusudia moyoni mwao ya kwamba walikuwa wamekubali huyo kuwa ni Mungu, na ni hayo tu.

29 Asubuhi moja watoto walikuwa wameenda shuleni, naye alikuwa amesimama akiosha vyombo. Na ilikuwa ni vigumu kwake kula chochote, kwa sababu hicho kidonda kingemchoma tu. Alikuwa akiosha vyombo, naye alisema mara ghafla hisia nzuri sana ilimjia. Naye akaendelea, akawazia, "Hiyo ilikuwa ni nini? Nilijisikia kigeni sana, mwepesi tu kabisa, na hisia nzuri." Vema, akaendelea tu kuosha vyombo.

30 Katika dakika chache, akashikwa na njaa sana, kwa hiyo akaenda me—mezani, nao watoto walikuwa wameacha uji wa shayiri kwenye sahani, kwa hiyo akachota kijiko kimoja cha uji huo, akanywa, halafu akauma tosti kidogo. Akawaza, "Vema, kama kawaida, nitakitapika, labda katika dakika chache."

31 Na kwa hiyo akaendelea, kwanza mwajua, ilikuwa ni sawa, akaendelea, akawa mzima. Kisha akaenda kule na kuonja tena, ilikuwa sawa. Ndipo kweli akawa na yubile ya mlo. Akaenda

na kujikaangia mayai kadhaa, kipande kikubwa cha nyama ya nguruwe, akachukua kikombe cha kahawa, na akala kwelikweli.

32 Akaendelea kuosha vyombo kwa muda kidogo, kisha akasimama kwa miguu yake, akajisikia mzima. Akainua mikono yake na kuanza kumsifu Mungu, akakimbia barabarani, alikuwa anaenda kumwambia dada yake kile kilichotukia. Alipofika kule chini, maskini mama huyu alikuwa akitembea sakafuni akitikisa shuka kwa nguvu alivyoweza. Kasema, "Vema, kuna nini, dada?"

33 Kasema, "Tazama! Kitu hicho kimetoka shingoni mwangu, siwezi kukipata kwenye shuka, siwezi kukipata mahali popote hata kidogo." Kilikuwa kimetoweka.

34 Ilikuwa ni kitu gani? Kwa sababu walishikilia hiyo hisi ya sita ya Neno la Mungu ambalo halingechukua hapana kama jibu. Jambo ndilo hilo. Walikuja mkutanoni yapata miezi miwili baadaye, wote wawili, wakanionyesha ninii . . . jinsi walivyoponywa na kadhalika. Ilikuwa ni kitu gani? Hisi ya sita, hiyo hisi ya sita, hiyo hisi ya nguvu, kitu hicho kilichowakomboa. Si kwa sababu niliomba, bali kwa sababu waliamini. Jambo ndilo hilo, hilo lilitosha.

35 Sasa, walikuwa huko juu kwenye Maskani ya Cadle huko Indianapolis, ama, ni kutoka hapa chini, hadi Indianapolis. Walikuwa na m—mvulana aliyekuwa na polio. Nao wakaleta . . . Baada ya yule msichana wa Rediger kuponywa . . . Msichana wa Ndugu Rediger alikuwa ameketi huko nje katika—katika kibanda cha makaa, akijaribu kumshikilia, alikuwa ameingia wazimu.

36 Ni wangapi wanaomkumbuka B. E. Rediger, mchungaji wa Maskani ya Injili ya Fort Wayne? Loo, nena kuhusu mtu aliyeamini katika uponyaji! Siku za Ndugu Bosworth. Hivi hamumkumbuki, Dk. Sullivan? Na mtu mzuri sana.

37 Basi binti yake aliyeketi huko nje alikuwa ameingia wazimu kwa ugonjwa wa akili ambao ulikuwa umemwua dada yake. Naye alikuwa ni mwanamke mrembo. Ilikuwa asubuhi ya Pasaka. Naye mama yake alikuwa ameketi huko nje. Basi nikiisha kumaliza mstari wa maombi, mtu fulani alisema, "Kuna mama mmoja hapa nje kwenye kibanda cha makaa, katika, kanisani pamoja na binti yake." Kasema, "Yeye ni Bibi B. E. Rediger kutoka Maskani ya Injili ya Fort Wayne."

38 Nikawaza, "*Ati nini*? Mke wa B. E. Rediger na binti yake wameketi kwenye kibanda changu cha makaa ya mawe?" Basi nikaenda huko nje, na hao hapo wameketi kwenye maskini mabenchi madogo, yalikuwa yametupwa kutoka kwenye shule ya Jumapili mle ndani pamoja na makaratasi. Msichana mrembo ameketi pale, mwenye umri wa kama miaka kumi na minane, ishirini, akizivuta nywele zake, namna *hii*, na kusema, "Nikeli ni nikeli. Peni ni peni. Nikeli ni nikeli. Peni iliyowekwa

akiba, peni—peni iliyopatikana, peni iliyowekwa akiba. Nikeli iliyopotea, nikeli iliyopotea.” Akiendelea namna hiyo, akivuta nywele zake, akiendelea.

Nikasema, “Bibi. Rediger,” nikasema, “wewe ni Bibi Rediger?”

Akasema, “Ndiyo.”

Nami nikasema, “Mimi ni Ndugu Branham.”

Akasema, “Vema, nina furaha kukutana nawe, Ndugu Branham.”

39 Nikasema, “Mume wako karibu alikuwa sanamu moyoni mwangu nilipokuwa mvulana mdogo. Ni mtu mashuhuri jinsi gani!” Akaanza kulia. Nikasema, “Huyu ni binti yake?”

Kasema, “Naam, Ndugu Branham. Tumekuwa naye kila mahali, hakuna kitu kinachoweza kufanyika. Naye dada yake, Romayne, alikufa.”

40 Nikasema, “Je, Romayne alikufa na huo?” Nikasema, “Nina picha zenu zote nyumbani na kadhalika, vitabu vyenu juu ya *Maji Yaliyo Hai*, na kadhalika, ambavyo Ndugu Rediger aliandika.” Nikasema, “Mbona, nilipokuwa hata mvulana, yeye alikuwa ni mtu mashuhuri, nilikuwa nikimsikiliza kwenye redio.” Nikasema, “Huyu ni binti yake?”

Kasema, “Huyo ni binti yake.”

41 Kitu fulani kikanijia, baba yake amekufa na kuzikwa, nikaenda kwenye, hiyo hisi ya sita ikaanza kusogea, nikasema, “Shetani, huwezi kumshikilia tena, katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yake!”

Kwa hiyo, mama akasema . . . nikasema . . . Yeye akasema, “Nifanye nini?”

Nikasema, “Amepona, mpeleke nyumbani.”

42 Alikuwa angali ameketi pale, “Nikeli ni nikeli, peni iliyopatikana, peni iliyopotea,” na kadhalika namna hiyo, akiendelea.

43 Wakampeleka nyumbani, na kesho yake akarudia fahamu zake, naye ni mwanamke aliyeolewa na ana watoto kadhaa sasa. Ilikuwa ni kitu gani? Kushikilia hiyo hisi ya sita.

44 Wakati fulani uliopita, kama ulitaka thibitisho la ushuhuda huu kile hisi ya sita itafanya, tulikuwa huko, nilikuwa pamoja na Ndugu G. H. Brown, Mtaa wa Victor 505, huko Little Rock, Arkansas, na kulikuwa na mmoja wa magonjwa mabaya sana niyowahi kuona maishani mwangu. Ndugu Brown, baada ya mimi kujaribu kuchukua pumziko dogo kutokana na kusimama kwenye mstari wa maombi kwa muda mrefu sana, alisema, “Ndugu Branham, chini kwenye orofa ya chini hapa,” kwenye jumba la mikutano, “ni moja ya vituko vya kutisha sana

ulivyowahi kuona." Kasema, "Mwanamke huyo aliponywa kichaa kutoka huko Mississippi."

45 Mvulana wake alikuwa askari, alikuwa huko kwa muda wa miaka ishirini, hata hakumjua mvulana wake, naye akapata akili timamu nilipokuwa nikimwombea. Hilo lilikitia tu moto kitu hicho.

46 Ndipo basi akasema, "Angalia haya." Nikashuka nikaenda kule, na ni mwanamke mkubwa, mzito, kijana, huku miguu yake imechomoza moja kwa moja juu, akiwa na nguo chache tu walizomvalisha hospitalini, maana hakusimama kwa miguu yake, hakuwa amesimama kwa miguu yake kwa muda wa miaka miwili, viungo vyake vilikuwa vinatokwa na damu, mikono yake ilikuwa ikitoka damu, naye alikuwa amelala huku miguu yote miwili imeinuliwa, na mikono yote miwili juu namna *hiyo*.

Ndipo nikamwambia huyo mtu, nikasema, "Vema, ana shida gani?"

47 Kasema, "Amerukwa na akili, Ndugu Branham. Alidungwa sindano, ndipo jambo fulani likampata," kasema, "mara baada ya mtoto wetu kuzaliwa," kisha kasema, "i—ilipoozesha kitu fulani akilini mwake." Kasema, "Amekuwa hospitalini sasa kwa miaka miwili." Naye akasema . . .

Nikasema, "Mbona anatokwa na damu *hivi*?"

48 Kasema, "Vema, wasingemruhusu atoke hospitalini." Kisha kasema, "Hawangetumia gari la kuchukulia wagonjwa, kwa sababu hana—hana akili timamu." Kisha kasema, "Nilimkodisha ndugu fulani achukue gari lake la Chevrolet halafu nikachukua wanaume wengine wanne, nasi tukajaribu kumshikilia kwenye kiti hicho cha nyuma, wanaume wanne, naye akapiga teke na kuvunja madirisha, na kadhalika, tukishuka kuja hapa." Karibu maili tisini kutoka kwenye hospitali alimotoka.

Nami nikasema, "Unamaanisha anatokwa na damu namna hiyo . . . ?" Nikasema, "Vema, nitaenda nimwekee mikono."

Akasema, "Loo, usifanye hivyo!" Kasema, "Angekuua."

49 Vema, nilikuwa tu mchanga hudumani, nami nimekuwa katika huduma kama hii kwa karibu, loo, nadhani, ilikuwa kitu kama mwaka mmoja, niliwaza, "Mungu, shughulikia jambo hilo." Nikatoka nikaenda sakafuni, naye alikuwa tu ameinua mikono yake juu, nikasema, "U hali gani, dada?"

50 Na lilikuwa ni jambo zuri kwamba nilikuwa mwangalifu, huo mkono mkubwa mno, wenye nguvu, wakipagawa na pepo wao wana mara kumi ya nguvu zao, naye akakutua *hivyo* kwa nguvu sana, akanirusha moja kwa moja kutoka kwenye miguu yangu. Basi alipofanya hivyo, mguu wangu uligonga moja kwa moja kifuani mwa—mwake *hapa*, ndipo nikauvuta na

kutoa mkono wangu, kisha nikamtoroka, na kukimbia kwenye kipandio namna hiyo, naye mumewe alikuwa amesimama hapo.

51 Naye akanifuata, akitambaa kwa mgongo wake kama nyoka, akipata wakati mzuri akinifukuza akitambaa kwa mgongo wake, huku ameinua mikono na miguu yake juu, akienda tu . . . Ningali ninaweza kusikia kelele hiyo ya kutisha, akijikokota kama nyoka, akipitia sakafuni. Alikuwa na uzito wa yapata ratili mia moja na sabini, naye alikuwa akijikokota namna hiyo.

52 Akaja moja kwa moja pale, akageuka, akaweka miguu yake mikubwa yenye nguvu ukutani namna hiyo, kisha akarusha mateke kwa nguvu sana, akagonga be—benchi lililowekwa pale nje, na kubandua ngozi kichwani mwake, sehemu ya ngozi ya kichwa chake imejimenya, damu ikaanza kutoka namna hiyo. Akachukua kijiti hiki kilichokuwa kimevunjika kutoka kwake, na kumtupia mumewe hicho, na kuangusha plasta yote kutoka ukutani, ilitubidi kuinamisha vichwa vyetu.

Akasema, “Nilikwambia.”

Nikasema, “Sijawahi kuona kitu kama hicho maishani mwangu.”

Akasema, “Ni kitu gani hicho, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Huyo ni ibilisi.”

53 Na papo hapo akatambaa akinijia, akasema, “William Branham, huna uhusiano wowote nami, nilimleta hapa.” Ndipo mumewe akaangalia, na kusema, “Mbona, hata hajui yeye ni nani! Imekuwaje . . . ? Hakujui.” Nami nikasema, “Huyo si yeye, huyo ni ibilisi, huyo ni yule ibilisi.”

54 Nami nikasema, “Shetani, unatambua na unajua ya kwamba sina mamlaka juu yako, lakini Bwana wangu anayo, kwa kuwa Yeye alikushinda pale Kalvari. Na kwa karama ya Kiungu niliyopewa na Malaika, ambaye aliniambia niwafanye watu wawe waaminifu na hakuna kitu kingesimama mbele ya maombi,” nikasema, “Katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yake!” Hakuna mabadiliko.

55 Maskini mumewe, amevaa ovaroli kuukuu, akanikumbatia shingoni, akaanza kunikumbatia, naye akasema, “Yanipasa nimfanyie nini, Ndugu Branham?”

Nikasema, “Mrudisheni hospitalini kama watampokea.”

Akasema, “Vema, waonaje?”

Nikasema, “Si vile nionavyo, ni vile uonavyo wewe?”

Akasema, “Ninaamini ya kwamba atakuwa mzima.”

Nikasema, “Hayo ndiyo yote unayohitaji kufanya.

“Naamini atakuwa mzima.”

56 Walipokuwa wakirudi usiku huo, hawakupata shida hata kidogo naye. Kesho yake asubuhi wakati ninii, walipokuja

kumchukua, alikuwa ameketi na akazungumza na matroni. Halafu siku ya pili akaruhusiwa kutoka hospitalini, mzima kabisa na mwenye afya.

57 Yapata miezi sita baadaye nilikuwa huko Jonesboro, Arkansas, pamoja na Richard Reed kwenye Maskani ya Old Fashion Revival Hour huko—huko Jonesboro, Arkansas. Ilikuwa ni maskani kubwa ya Kibaptisti, huketi watu wengi zaidi ya hii hapa, mahali hapa. Basi nilikuwa ninaanza kuhubiri, nami niliendelea kumwona mtu fulani akinipungia mkono huko nje, nami sikujua alikuwa ni nani.

58 Naye asingeweza kuvumilia hilo tena, akasema, "Unanikumbuka?" Alikuwa na watoto wadogo wanne ama watano.

Nami nikasema, "Siamini nakukumbuka."

59 Akasema, "Wala nami sijawahi kukuona hapo awali," akasema, "lakini nilikuwa yule mwanamke aliyekuwa amelala kichalichali, akitambaa." Naye mumewe katika muda huo wa miezi sita alikuwa ameitwa hudumani, naye alikuwa akitoka kwenda kuihubiri Injili. Loo, jamani!

60 Ni kitu gani? Kushikilia hisi hiyo ya sita. Imani ilisema hivyo! Akasema, "Niliweka jambo hilo moyoni mwangu. Kama Mungu angeweza kuwafanyia wengine jambo kama hilo, Yeye anaweza kumfanyia mke wangu." Akaendelea kushikilia hilo, hakuna kitu kingalimtenga nalo. Hivyo ndivyo hiyo hisi ya sita itakavyofanya ikiachiliwa, na kuiacha iwe na nguvu zake za kutawala.

61 Usiku mmoja nilikuja nyumbani, nilikuwa nimelala kitandani mwangu. Kama mkitaka kuandika mpate shuhuda hizi, ninawapa anwani. Mwandikie Georgia Carter, Milltown, Indiana, na ita—itamwendea: Georgia Carter, Milltown, Indiana. Naye alikuwa mfuasi wa kanisa ambalo halikuamini katika uponyaji wa Kiungu.

62 Alikuwa akifanya masomo ya piano alipokuwa msichana mdogo, naye mjomba wake alikuwa akimpeleka kwenye hili, kwenye somo la piano, na alipofanya hivyo, mtu huyu, akiwa mtu mzima, naye ni msichana mdogo, alimbaka huyo mtoto, basi alipofanya hivyo, ikamwambukiza TB. Naye alikuwa amelala kichalichali miaka tisa na miezi minane akiugua TB ya tezi za kike, kote mwilini mwake hata kwenye mapafu yake. Naye, takriban, alikuwa na uzito wa ratili thelathini na saba, nafikiri, hivyo, kile walichoweza kumpima.

63 Sasa, unaweza tu kumwandikia ukitaka, ni majaliwa yako, atafurahia kukujibu. Nami sikujua lolote kumhusu msichana huyo. Wala hata sikujua Milltown ilikuwa wapi.

64 Ndipo nikaingia nyumbani na kumwona Mama, nami nikasema, “Ninaenda kulala mapema usiku wa leo, kwa sababu ninataka kuingia na kutafakari juu ya Bwana.”

Akasema, “Vema, Billy, ingia tu, nenda ukalale.”

65 Nikaingia chumbani, nami nikaomba, na kuomba kwa muda mrefu. Ndipo baada ya kitambo kidogo nikaangalia kule... Naye Mama alikuwa tu mmoja wa hawa wanawake wa mtindo wa kale, wa mashambani, anafua nguo zake na kuziweka kitini, sijui kama ninyi wanawake mliwahi kufanya hivyo au la, na kuziweka pale mpaka atakapozipiga pasi, anasimama miguu mitupu na kupiga pasi. Na kwa hiyo mimi...Mama alikuwa na viti vilivyowekwa pale, vimejaa nguo zetu sisi wavulana wote, nyumbani. Nami nilikuwa nikikaa nyumbani wakati huo, ilikuwa ni baada ya kumpoteza mke wangu kwa muda mrefu. Ndipo nikaangalia, na ilionekana kana kwamba kiti hicho kilikuwa kikija kunielekea mimi.

66 Basi nilipoangalia ilikuwa ile Nuru ikija kunielekea mimi. Ndipo ilipokuja papo hapo kwangu, nikaanza kana kwamba ninapitia nyikani, nami ningeweza kusikia kitu kama mwana-kondoo mdogo akilia, “*Mee*, *mee*.”

67 Ndipo nikawazia, “Loo, maskini jamaa huyo mdogo amenaswa mahali fulani.” Nami nikaanza kupitia kichakani nikijaribu kumtafuta. Basi nilipofika hapo, hapo karibu naye, ningeweza kusikiliza tena, nikasema, “Yuko wapi?” Nikawaza, “Maskini huyo mtoto!” Nami nikaanza kusogea karibu, karibu zaidi, nikipitia kichakani.

68 Basi alipokuwa akilia “*Mee*,” alikuwa akisema, “*Milltown*, *Milltown*.”

69 Nami nilikuwa nikifanya kazi, nikijaribu kumfikia, ndipo nikatoka kwenye lile ono. Nikawaza, “Milltown iko wapi?” Nikawazia, “Kuna shida huko Milltown, mwana-kondoo fulani amenaswa huko chini, ama, huko juu, popote alipo.”

70 Ndipo nikatoka, nikaliuliza kanisa langu Jumatano usiku, walijua mahali popote panapoitwa Milltown. Hakuna mtu aliyepajua. Vema, ndipo Jumapili nikauliza tena, “Kuna yeyote anayejua mahali panapoitwa Milltown?”

71 George Wright, wengi wa watu wangu hapa kutoka maskanini wanamjua George Wright, amekuwa akija kule kwa miaka mingi, akasema, “Mbona, Ndugu Branham,” kasema, “Milltown iko tu huko chini Kusini, yapata maili thelathini na tano kutoka hapa, mji mdogo, uko juu ya kilima kidogo kule chini.” Kasema, “Ninajua mahali ulipo.”

Nikasema, “Utanipeleka huko?”

Akasema, “Nitakupeleka.”

Vema, ndipo nikasema, “Nitakuwa huko Jumamosi ijayo.”

72 Vema, nikaenda Milltown, tukaenda huko, wana yapata maduka mawili tu ya vyakula. Nami niliwaona watu wakija katika mikokoteni yao na mabehewa, kama wafanyavyo huko chini Kentucky, mwajua, huko chini vilimani. Nami nikawaza, "Vema, sioni chochote hapa." Nikaingia na kumwuliza huyo mtu kama ningeweza kununua hilo sanduku dogo la mbao kutoka kwake.

Akasema, "Naam, unalitaka la nini?"

Nikasema, "Kuna watu wengi sana wanaosimama hapa nje, ninataka kujitengenezea jukwaa la kusimamia, mimi ni mhubiri, ninataka kuhubiri."

Akasema, "Sikudai chochote kwa ajili yake. Lipeleke huko nje, hiyo ni sawa."

73 Na kwa hiyo nikachukua sanduku langu, ndipo nilipochukua sanduku langu na kuondoka, nikamwona Ndugu Wright akija huko, akasema, "Ndugu Branham, sina budi kufanya biashara fulani juu ya hiki kilima hapa." Kasema, "Ukitaka, unaweza kwenda pamoja nami."

Nikasema, "Vema. Nitaweka tu kijisanduku changu hapa chini, kutakuwa na umati mkubwa zaidi kidogo, wakati nitakaporudi."

74 Ndipo nikapanda kilima, na tukapita karibu na maskini kanisa kubwa jeupe, nikasema, "Ni kanisa la aina gani hilo?"

75 Akasema, "Hilo ni kanisa la kale la Kibaptisti." Kasema, "Huyo mhubiri alipata shida fulani, na," kasema, "aligeuka kuwa jambazi, na kumbaka mke wa mtu fulani, nao wakampiga risasi, mambo mengi sana yaliendelea." Kasema, "Kusanyiko limetawanyika." Kisha kasema, "Hawaendelei na kanisa tena."

76 Vema, nikaanza kulizunguka hilo kanisa pamoja naye, basi nilipofanya hivyo, Kitu fulani kikasema, "Nenda kwenye kanisa hilo."

77 Nami nikaenda pale, naye. . . Nikasema, "Hebu nisimame hapa mpaka upande juu ya kilima."

Akasema, "Vema."

Nikasema, "Kwani hawana kanisa hapa?"

"La."

78 Nikajaribu kufungua mlango, wala huo mlango usingefunguka. Nikasema, "Baba wa Mbinguni, kuna jambo fulani kuhusu kanisa hili, ndiyo sababu umeniita sasa hivi? Je, kanisa hili ndilo lililonaswa kichakani? Hili ndilo unalopigia makelele, 'Milltown'? Kama hapa ndipo unaponitaka, nifungulie mlango huo." Nikaushika huo mlango, usingefunguka. Vema, nikaketi chini kwenye ngazi.

79 Na yapata tu wakati huo, mtu fulani akaja akitembea kulizunguka kanisa, akasema, "U hali gani?"

Nikasema, "U hali gani, bwana?"

Akasema, "Ulitaka ndani ya kanisa?"

Nami nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Nina ufunguo." Akafungua mlango.

Nikaangalia kote mle ndani, nikasema, "Ni mali ya nani?"

Kasema, "Huu mji."

Nikasema, "Sijui kama wanaweza kufanyia mikutano hapa?"

Kasema, "Nenda kwenye machimbo, ukawaulize."

80 Nami nikaenda kule, naye akasema . . . Nikasema, "Ninafanya kazi kwenye Mashirika ya Umma, nitaweka mita ndani yake, ningependa kufanyia ibada kadhaa mle."

Kasema, "Karibu, hakuna kodi kwake hata kidogo," kasema, "litunze tu."

Nami nikasema, "Asante, bwana, nitafanya hivyo."

81 Nami nikaenda kule, na kuweka mita, nikaanzisha uamsho. Usiku wa kwanza pale nilihubiri, "Mungu ni . . . Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu anabaki Mungu."

82 Naye Ndugu Hall, mtu fulani aliandika kipande kidogo mle ndani, ama, si Ndugu Hall, Ndugu Wright aliandika kipande kidogo mle ndani na kusema, "Njoo, usikie Billy Sunday mdogo."

83 Vema, usiku huo nilikuwa na kusanyiko kubwa: Bw. Wright, binti zake wawili, na mwanawe, kanisa litakaloenea yapata watu mia tano. Vema, nilihubiri kwa bidii nilivyoweza.

84 Usiku uliofuata nilikuwa na kusanyiko lile lile. Papo hapo yapata wakati nilipokuwa tayari kuninii, nikiketi nyuma ya mimbara kitini, nilikuwa nikitaka kuanzisha—kuanzisha ibada, nikasambaza vitabu vya nyimbo, vilikuwa vimetapakaa kila mahali, nikavipangusa vumbi. Nilifanya kazi kwa bidii siku nzima, kisha nikaingia, nikavipangusa vumbi. Nikaanza kushuka, vitabu hivi vya nyimbo, pamoja na vitabu hivi vya nyimbo, nikampa Ndugu Wright kimoja, hao wengine kimoja, nikarudi na kuketi chini. Yapata wakati huo nikasikia kitu fulani kikifanya [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] mlangoni. Nikaangalia, na huyu hapa jamaa mmoja akaingia.

85 Ndugu Wright akasema, "Loo, jamani!" Kasema, "Huyo hapo mnafiki na kafiri mkubwa kuliko wote aliyeko nchini."

86 Ndipo akamwaga kiko chake cha gunzi la hindi kando ya nyumba, akaingia namna hiyo, jino moja limetokeza, nywele zake zimening'inia machoni mwake, kasema, "Yuko wapi jamaa huyo anayeitwa, Billy Sunday mdogo?"

Nikarudi nyuma, nikasema, "Jina lako, bwana?"

Akasema, "Mimi ni Bill Hall, muuza maua hapa juu."

Nikasema, "Vema, mimi ni Ndugu Branham."

Akasema, "Je, wewe ndiwe yule Billy Sunday mdogo?"

87 Nikasema, "Hilo lilikosewa." Nikasema, "La, mimi siye Billy Sunday mdogo." Nikasema, "Hivi hutakuja hapa mbele na kuketi chini?"

Kasema, "Nitaridhika papa hapa nyuma."

Nikasema, "Vema, jisikie nyumbani. Hiki hapa kitabu cha nyimbo."

Kasema, "Sijui kuimba."

Nikasema, "Vema, wala sisi pia, bali tutampigia Bwana kelele za shangwe."

88 Nikapanda juu, nikahubiri. Nilipoanza kuhubiri, aliendelea kusonga mbele kidogo, mbele kidogo, ndipo nilipotoa wito wa madhabahuni, alikuwa madhabahuni, kisha akawa mchungaji wa kanisa hilo mpaka sasa. Mnaona?

89 Sasa, siku chache baadaye nikaanza kuhubiri juu ya uponyaji wa Kiungu. Wakaniambia kuhusu msichana aliyeishi juu ya kilima ambaye alikuwa amelala kitandani miaka tisa na ninii sita. . . na miezi minane bila hata kuona nje.

90 Vema, ni—nikasema, "Vema, sijui. Ninii. . . ikiwa. . . " Mchungaji wao alikuwa tayari ametangaza katika kanisa fulani la kimadhehebu lililosema, "Siku za miujiza zimepita." Karibu makanisa yote karibu na hapo yalisema, "Kama mtu yeyote akienda kule, wewe kwanza kabisa umetengwa." Kwa hiyo, baba yake alikuwa shemasi katika kanisa hilo. Kwa hiyo ilikuwa ni vigumu kwao, kuja kule juu.

91 Nacho kitabu changu kidogo, wengi wenu huenda mmekisoma kiitwacho *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*, vema, kuna. . . maskini ushuhuda wa msichana wa Nail uko mle ndani ambapo alikuwa ameponywa.

92 Vema, waliagizia niitwe nije, nimwombee msichana aliyekuwa na TB, nao wazazi wake walinitaka nije. Nikapanda nikaenda nikamwombea, akarudi pamoja nami kanisani humo usiku huo, alikuwa amelala pale kwa muda mrefu.

93 Georgia akasikia habari hii, naye akaanza tu kulia. Hatimaye, mama na baba yake walikubali kwamba ningeweza kuja kumwombea, lakini hata wasingekuwa ndani ya nyumba, wakaenda zao, wakaenda zao.

94 Kwa hiyo nikaingia, maskini huyo mtoto, angejaribu kukohoa, angefanya, "*Humfu-humfu! Humfu-humfu!*" Asingeweza kushikilia kikombe chake cha makohozi apate kutemea. Naye akasema, "Ni. . . nilisoma. . . kile kitabu. . . kidogo." Ndipo nikaangalia na kulikuwa na picha yangu na kile kitabu kidogo kiitwacho *Yesu, Yeye Yule Jana, Leo,*

*Na Hata Milele*. Naye akasema, "Mimi. . .ninaamini. . .Yeye ataniponya."

95 Ndipo nikasema, "Vema, sitaki kusababisha msuguano kanisani mwenu, ewe msichana. Lakini wako wapi baba na mama yako?" Machozi, alikopata unyevu wa kutosha kutoa machozi, sijui, yakatiririka chini ya uso wake ambapo hata ungeweza kuona mahali fuvu la kichwa chake lilipounganishwa. Alikuwa mfuasi wa kanisa maarufu sana linalokana nguvu za Mungu. Hawaninii. . .Farisayo mambo leo tu, hawaamini katika Roho Mtakatifu, hakuna chochote; batizwa tu majini na uwe mfuasi wa kanisa. Na kwa hiyo, sikutaka kusababisha hisia zozote kali miongoni mwa watu.

Nami nikasema, "Vema sasa, nitakuombea."

Naye akasema, "Je, utafanya kama ulivyomfanyia yule msichana wa Nail?"

96 Nikasema, "Dada, hilo lilikuwa ni ono, ninaweza tu kufanya kama Mungu asemavyo nifanye." Basi nikamwombea, hakupata nafuu hata kidogo. Nikamaliza uamsho wangu, nami nilikuwa na yapata sitini ama sabini na watano wa kubatizwa mwishoni mwa juma hilo, naye alimwahidi Mungu kama angeweza kuponywa, angeenda akabatizwe, huko juu mahali panapoitwa Totten Ford katika Mto mdogo wa Blue kule.

97 Vema, siku, siku ya kubatizwa ilipowadia, nilitoka nikaenda kule nje. Basi kulikuwako na mhubiri, alikuwa amenidhihaki juu ya ubatizo wa maji. Loo, jamani, jamani! Naye alikuwa na uamsho wa hema kwenye kilele tu cha kilima hicho. Basi nilipokuwa huko nje majini nikibatiza, nilisema, "Inaonekana tu kwangu kwamba Malaika wa Mungu wameketi huku." Na kila mmoja wa kusanyiko lake, yale maji yaliyojaa matope huku wamevaa nguo nzuri nyeupe, alitoka akaenda kule na kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo, kila mmoja wao. Hiyo ni kweli. Loo, ni wakati wa jinsi gani!

98 Tukaanza kwenda kwa Bw. Wright kula chakula cha jioni. Basi nilipofanya hivyo, nikasema, "Sijisikii kula chakula cha jioni kabla sijarudi mkutanoni usiku wa leo, ninaamini nitapanda huko na kuomba, nina mzigo moyoni mwangu kwa ajili ya msichana huyo mdogo."

99 Nami nikapanda kule juu, na, ubavuni mwa kilima nikaanza kuomba. Yapata majuma machache yaliyopita nilikuwa kule chini, kichaka kile kile kidogo. Nilikuwa nimepiga magoti pale nikiomba, nikimtazamia Mungu. Najaribu kutulia, ndipo kungekuwa na waridi mwitu kando ya mguu wangu, ikinikwaruza, ninii tu. . .Mnajua, hebu anza tu kuomba ama kufanya jambo sahihi, na uangalie jinsi ibilisi anavyokushika. Nami nikarudi huku, na machweo ya jua yalikuwa yakiangaza machoni mwangu, nikarudi upande huu, kila mahali ulipokuwa. . .basi hatimaye nikakata tamaa tu,

nami nikasema, "Bwana Mungu, acha vijiti vichome magoti yangu, ama mawe yaumize magoti yangu, ama chochote kile, ninaomba." Ndipo nikaanza kuomba.

100 Yapata tu wakati nilipoanza kuomba vizuri sana, nikaangalia, na kutoka kwenye kichaka kidogo cha dogwood . . . Kuna mtu anayejua dogwood ni nini? Loo, hakika, Ohio inajua dogwood ni nini. Na kichaka kidogo cha dogwood pale, ile Nuru, yule Malaika wa Mungu, ambaye picha Yake mnayo hapa, hiyo Nuru ilikuwa inaangaza chini kutoka kwenye kichaka hicho, kasema, "Simama kwa miguu yako."

Nikasema, "Naam, Bwana wangu."

Kasema, "Shika njia uende kwa Carter." Hayo tu ndiyo aliyosema.

101 Vema, wakati ni—nilipokuwa nimesikia hiyo kengele ikilia, naye Bw. Wright akaniambia, kasema, "Sasa wakati hiyo kengele ikilia, Mama ameweka chakula cha jioni mezani, basi uje," kengele ya kale ya mashambani, kasema, ukiipiga, "wakati anapoipiga, wewe njoo." Niliisikia, bali nilikuwa katika ono, wala nisingeweza kwenda.

102 Mnajua Mungu hujibu pande zote mbili za mstari. Hivi hamwamini hilo? Wakati uo huo, maskini Georgia alikuwa na wasiwasi sana, akijua nitaondoka nchini, alikuwa akilia, naye alitaka kuja na kubatizwa, naye alikuwa amemwahidi Mungu, akahangaika sana.

103 Naye mama yake, mwanamke mzuri sana, basi akatoka akaenda jikoni, akapiga magoti, na kufunga mlango kati yake na Georgia, naye akasema, "Ee Mungu wa Mbinguni," akasema, "mfanyie jambo huyo mdanganyifu duni, ambaye amepitia nchini mwetu hapa. Katika miaka tisa ambayo maskini msichana wangu mdogo amelala kwenye kitanda hicho, hajawahi kulalamika hata wakati mmoja, na sasa amemvuruga kabisa akilini mwake, akimwambia kuhusu Mponyaji, ama *kitu kingine*."

104 Kisha kasema, "Mkemee mtu huyo! Mkemee mtu huyo, Bwana!" Alikuwa mwaminifu kulihusu. Akasema, "Mfukuze nchini. Maskini msichana wangu mdogo amelala mle ndani akifa bila tumaini kwamba anaweza kuishi tena mle ndani, na kulala mle ndani namna hiyo, halafu huyo mdanganyifu anamchochea kabisa chini ya tumaini la uwongo!"

105 Akasema, sasa, huu ndio ushuhuda wake, sikuwako, akasema alisimama, alifikiri alimsikia mtu akija, akasimama. Binti yake aliishi kilimani mbali kidogo, naye alidhani ilikuwa ni binti yake. Akatazama nyuma, akatazama, na kusema ukutani, mahali ambapo jua lilikuwa linatua, wakati uo huo nilipokuwa nikiomba, akaona kivuli kikishuka ukutani, ilikuwa ni Yesu, akasema.

106 Kasema, “Huyo hapo akiwa na sura nzuri tu kadiri ulivyowahi kuona, pamoja na ndevu Zake. Akasema, ‘Mbona unalia? Ni nani huyu anayekuja?’” Kasema aliangalia hapa na akaona kivuli changu, kidogo nina upara kwa sehemu kichwani, nimebeba Biblia ii hii hapa kwenye moyo wangu, nikija, nikitembea huku mtu fulani akinifuata.

107 Naye akaingia mbio, akasema, “Georgia, jambo la kiajabu sana lilitukia.” Akasema, “Hapana shaka nilishikwa na usingizi, nikaota ndoto, nikamwona yule mhubiri akija.” Na yapata wakati huo, mlango wa gari ukafungwa, nilikuwa nikitoka nje.

108 Loo, Mungu hujibu pande zote mbili kama tu utamruhusu afanye hivyo. Kulikuwako na Georgia kule akiamini dhidi ya kutokuamini kwote, alikuwa bado anashikilia kwamba Mungu angemponya, kwamba angaliweza kumponya msichana mmoja, angeweza kumponya mwingine. Naam.

109 Ndipo akaniona. Nami nikaenda chini ya upako, hata sikubisha mlangoni, nilifungua tu mlango. Baba yake alikuwa ameenda kwenye kibanda chake kuleta maziwa, ndiyo kwanza amalizie kukamua maziwa. Na kwa hiyo nikaenda pale, nikafungua mlango, nikaingia mle, mimi . . . Ndipo mwanamke huyu, huyo mama, akazimia tu na kuanguka sakafuni. Naye Georgia alikuwa pale, naye akaniangalia.

110 Nami nikasema, “Dada Georgia, Bwana Yesu Kristo, ambaye ndani Yake unapenda . . . ” Na pale nyuma ya kitanda, kile kitanda kidogo alichokuwa amesugua rangi yake yote mradi tu angeweza kurudisha mikono yake huko nyuma, akishikilia hicho, na kumlilia Mungu apate nafuu; huku kanisa lake likimwambia ya kwamba siku za miujiza zimepita. Alizaliwa apate kuwa mtoto wa Mungu.

111 Hapo, yeye alikuwa akishikilia ahadi hiyo, Mungu kwa rehema Zake alionyesha ono na kunituma kule chini, ilikuwa ni huko. Nikasema, “Ninajua wewe ni nani sasa, wewe ndiye yule mwana-kondoo niliyemwona ameshikwa kwenye lundo hili la theolojia hapa chini.” Haleluya!

112 Nikasema, “Georgia, Bwana Yesu unayempenda na kumtumikia alinitokea hapa juu kilimani muda mfupi uliopita, na Nuru ile ile iliyotanda juu ya yule msichana wa Nail, Naye akaniambia nipitie huku. Ninamwamuru ibilisi katika Jina la Yesu Kristo akuache!” Nikasema, “Simama kwa miguu yako.”

113 Shetani akasema, “Atasimamaje, na miguu yake hata si mikubwa kuliko kijiti cha ufagio, angalau?”

114 Hilo halikuwa wazo. “Njoo huku, kwa vyovyote vile!” Wala hata asingeweza kuinua kikombe chake cha makohozi.

115 Naye akainuka kutoka kwenye kitanda hicho chini ya nguvu za Roho Mtakatifu, akatembea kwenye sakafu hiyo, akimsifu Mungu, akatoka akaketi chini uani, na kubariki nyasi,

na majani, na kadhalika, hakuwa ameyaona kwa miaka tisa. Nikageuka, nikaondoka.

116 Mama yake akasimama na kuanza kupiga mayowe na kuanguka, kisha akaanguka barazani na huko nje uani. Majirani wakaanza kuja, wakidhani huyo msichana alikuwa amekufa, ama kitu fulani. Naye huyu hapa uani, akitembea huku na huku, akipigapiga majani na kumsifu Mungu.

117 Baba yake akasikia kelele hizo zote kwa hiyo akashuka akaja. Huyo hapo mke wake amelala, nao watu wakimpepea namna hiyo, kisha akasikia kinanda kikicheza. Naye akaingia ndani ya nyumba, huyo hapo maskini binti yake, ameketi kwenye kinanda akicheza:

> Kuna chemchemi iliyojaa Damu,
> Iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli,
> Wenye dhambi wakitumbukizwa chini ya hiyo
> gharika,
> Hupoteza madoa yao yote ya hatia.

118 Loo, jamani! Hajawa kitandani zaidi ya kwenda kulala usingizi tangu wakati huo, hiyo imekuwa miaka kumi na mitano, kumi na sita iliyopita. Loo, ilikuwa ni nini? Akishikilia hiyo hisi ya sita, *kitu fulani* ndani kikisema, "Kama angeweza kumponya mmoja, anaweza kuniponya." Haleluya! Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli.

119 Nakumbuka hapa juu Fort Wayne, mzee John Rhyn, si yule mtu mwenye masharubu, yule mwingine, kipofu John Rhyn, Nilikuwa na mkutano huko juu katika maskani kubwa. Niko karibu kufunga, nianze kuwaombea wagonjwa. Mtu huyu alikuwa ameketi kwenye roshani, alikuwa Mkatoliki, walimleta madhabahuni, wakamleta jukwaani kwa kadi yake.

120 Alipofika mahali nilipokuwa, kasema, "Jina lako ni John Rhyn."

"Hiyo ni kweli."

"Nawe ni Mkatoliki kwa imani."

Akasema, "Hiyo ni kweli."

"Ulikuwa ukiendesha kwenye sarakasi."

"Hiyo ni kweli."

Kasema basi, "Na umekuwa kipofu sasa kwa miaka ishirini na kitu, ama zaidi."

Kasema, "Hiyo ni kweli."

121 Na namna fulani ya lukemia, ama *kitu kama hicho*, iliingia machoni mwake na kumpofusha. Nikasema, "Wewe ni ombaomba."

Naye akasema, "Si ombaomba hasa, bali," kasema, "niliketi mtaani."

Nami nikasema, “Vema, hilo ni sawa.” Nikasema, “Je, unaamini ya kwamba Yesu Kristo atakuponya?”

Akasema, “Ninaamini.”

122 Nikamwombea, na kumwekea mikono, nikasema, “Bwana Yesu, ninakemea upofu huu sasa, katika Jina la Yesu Kristo, na umwache.” Nikageuka na kuangalia, nikamwona akienda zake huku anaona. Nikasema, “BWANA ASEMA HIVI,” hebu angalieni hilo, “BWANA ASEMA HIVI, umefumbuliwa macho.”

Vema, a—akasema, “Siwezi kuona.”

Nikasema, “Hilo halina uhusiano wowote nalo. Nenda zako ukishangilia.” Kwa hiyo akashuka akaenda.

123 Kulikuwa na mwanamke katika dakika chache, alikuwa na tezi kubwa ikining’inia kooni mwake, na tulipokuwa tukimwombea ikatoweka. Huyu hapa John Rhyn anarudi, akisukuma mabawabu wote, akirudi tena. Na kwa hiyo, yule mtu aliyekuwa akinisaidia kwenye mstari wa maombi, akaanza kumwondosha jukwaani. Akasema, “Ninataka kumwona mhubiri huyo.” Na kwa hiyo wakamleta pale tena. Akasema, akaniambia, akasema, “Uliniambia nimeponywa.”

Nikasema, “Umeponywa.”

Akasema, “Vema, kama niliponywa, ningeweza kuona.” Akasema . . .

Nikasema, “Loo, la, hilo halina uhusiano wowote nalo. Uliniambia . . . ”

Akasema, “Vema, ulisema niliponywa.”

Nikasema, “Ulisema uliniamini.”

Akasema, “Ninakuamini.”

Nikasema, “Basi kwa nini unatilia shaka?”

Akasema, “Vema, kama niliponywa, si ningeweza kuona?”

124 Nikasema, “Utaona. Mungu aliponionyesha ono kwamba ulikuwa unaona, halina budi kutukia.” Alikuwa Mkatoliki, wala hakuwa amewahi kufundishwa chochote kama hicho.

Akasema, “Lakini sielewi. Nifanye nini?”

Nikasema, “Vema, jambo pekee la kufanya ni kwenda zako ukimsifu tu Mungu kwa kuyafumbua macho yako.”

Akasema, “Uko wapi?” Akaanza kusukuma mbele, kasema, “Ngoja kidogo.” Kasema, “Jina lako ni nani?

Nami nikasema, “Branham.”

125 Akasema, “Hebu nikuguse.” Nami . . . akaiweka mikono yangu juu yake. Akasema, “Bw. Branham, kama Mkatoliki, nimefundishwa kumwamini kasisi wangu.” Naye akasema, “Nimekuja kwako kuomba usaidizi, nawe ukaniambia mimi ni nani na yote kuhusu hali zangu, kile ambacho hakuna mtu

ajuaye ila Mungu, ninaamini kwamba ni kweli, nitaendelea kusema, 'Mungu asifiwe.'" Huyo akaondoka jukwaani.

126 Mbona, ilikuwa vigumu kwangu kufanya ibada siku mbili zilizofuata usiku, angesimama kila mahali, akipaza sauti, aseme, "Bwana asifiwe kwa kuniponya!" Nami ningeanza kuhubiri, angesimama pale, na kupaza sauti, "Bwana asifiwe kwa kuniponya!"

127 Wakampa kazi ya kuuza magazeti. Karibu mwezi mmoja ulikuwa umeisha, akipaza sauti, "Bwana asifiwe kwa kuniponya!" Naye alikuwa kule chini, ndipo akapaza sauti, "Ziada! Bwana asifiwe kwa kuniponya!"

128 Wakamcheka, wakamdhihaki, wavulana wadogo wauza magazeti wakamzomea, watu mitaani wakasema, "Mzee huyo amerukwa na akili."

129 Naye angesema, "Ziada! Ziada! Soma yote kuyahusu! Bwana asifiwe kwa kuniponya! Ziada! Soma yote kuyahusu! Bwana asifiwe kwa kuniponya!"

130 Wakamchukua, nao walidhani itawabidi kumpeleka kwenye hospitali ya wendawazimu, basi wakamhoji, akasema, "Mimi nina akili timamu tu kadiri nilivyowahi kuwa, bali ninamwamini Mungu. Bwana asifiwe kwa kuniponya!" akiendelea namna hiyo.

131 Ilikuwa ni kitu gani? Alikuwa ameshikilia hiyo hisi ya sita, kitu fulani ndani yake kikiishikilia hiyo. Hakuwa akitilia maanani kama angeweza kuona, macho hayo hayakuwa na uhusiano wowote nayo, alikuwa akiona kwa macho mengine, alimwona Mungu.

132 Tunaangalia vitu tusivyoviona. Silaha zote za Kikristo ni kwa imani. "Yeye amjiaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko." Matunda yote ya Roho, kila kitu ni imani, yasiyoonekana, tunaangalia yasiyoonekana. Tunaangalia yasiyoonekana, kwa imani tunayaona. Haleluya!

133 Maskini mvulana mdogo alimvusha barabarani apate kunyolewa kwa kinyozi. Ndipo maskini kinyozi fulani mjuaji alitaka kumdhihaki, kwa hiyo akaupaka uso wake sabuni vizuri, pamoja na vinyozi wengine, naye akawakonyezea macho namna *hiyo*, akasema, akaanza kumnyoa, akafika nusu upande kwenda chini, alikuwa ameweka taulo hapo juu, mwajua, naye akasema, "Aisee, Papa Rhyn."

Akasema, "Naam, mwanangu?"

Kasema, "Nilisikia ulienda kule kumwona yule mtakatifu anayejibingirisha alipokuwa hapa juu."

"Naam, nilienda," akasema.

Akasema, "Uh, nilisikia ya kwamba u—uliponywa."

134 Akasema, “Naam, niliponywa. Bwana asifiwe kwa kuniponya!” Basi alipofanya hivyo, macho yake yakafunguka kwenye kiti cha kinyozi. Huyo akaruka kutoka kitini mwake amejifunga taulo shingoni mwake, kinyozi akakimbia mlangoni ameshika wembe mkononi mwake. Mzee Rhyn akashuka mbio barabarani alivyoweza kwenda, akipiga mayowe na kupaza sauti, “Bwana asifiwe, ameniponya!”

135 Ilikuwa ni kitu gani? Kushikilia hiyo hisi ya sita, hicho ni kitu kinachoifanya halisi. Naam bwana. Kupitia hisi hii ya sita falme zimetiishwa. Amina. Hisi ya sita ilitiisha falme. Kupitia hisi hiyo ya sita kuta za Yeriko zilianguka chini kabisa. Amina. Mnaamini hilo? Kuta za Yeriko ziligonga chini, kupitia hisi ya sita.

136 Kupitia hisi ya sita ile bahari haingeweza kumzamisha Paulo. Aliposhuka kwenda kule, wakati matumaini yote yalipokwisha, aliona ono la Malaika wa Bwana, akarudi huku akisema, “Uwe na moyo wa ushujaa.” Kulikuwa na shida gani? Hakuna mwezi wala nyota kwa siku kumi na nne mchana na usiku, ilikuwa giza tu kama ilivyowahi kuwa, dhoruba ilikuwa kubwa tu kama ilivyowahi kuwa, lakini hiyo hisi ya sita ilianza kufanya kazi wakati alipomwona Malaika wa Bwana. Haleluya!

137 Hiyo hisi ya sita isingeweza kumweka Petro gerezani. La, bwana. Nguvu za Mungu zilimtuma Malaika mle ndani na kumkomboa.

138 Hisi ya sita haingeweza kuwaweka Paulo na Sila kifungoni. Mungu alituma tetemeko la ardhi, na kutikisa na kuangusha kitu hicho chote.

139 Hiyo hisi ya sita, hebu ifanye kazi kwako siku moja. Kwa sababu ya hisi hiyo ya sita simba hata hawakuweza kumla Danieli; hawangeweza kucheza na hiyo hisi ya sita. La, bwana.

140 Kwa hisi hiyo ya sita moto haungeweza kuwateketeza wana wa Kiebrania.

141 Kwa hisi ile ile ya sita iliyokuwa ikifanya kazi katika mtoto Martha, wakati alipokuja kumwona Yesu akimfufua ndugu yake kutoka kaburini, baada ya kufa kwa siku nne.

142 Hisi iyo hiyo ya sita ilimsafisha mwenye ukoma.

143 Hisi iyo hiyo ya sita ilimfufua Yesu Kristo katika siku ya tatu.

144 Hisi iyo hiyo ya sita italinyakua Kanisa moja ya siku hizi na kuliondoa hapa hadi Utukufuni.

145 Usizitegemee hizo tano, ni danganyifu, lakini hiyo ya sita ni sahihi. Ukitaka . . . Kuna jamaa mdogo hapa usiku wa leo, sijui kama Charlie Cox yupo hapa au la, nilikuwa nikizungumza naye juu ya hisi ya sita. Akaichukua hiyo, na kuiamini, na kuicheza kwenye kanda. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

146 Mke wake akasema, “Hebu niicheze.” Akamfukuza chumbani, naye akaanza kuicheza. Akasema, “Bwana, nina hisi ya sita, pia, nami nitaiweka kazini, ninamtaka Roho Mtakatifu,” naye Huyu hapa anakuja.

147 Ni kitu gani? Kama unaamini, ukiona, inatupasa kuamini bila kuona, lakini hata hivyo Mungu hutujalia kuiona, kwa vyovyote vile. Yeye anatuonyesha, na kutuonyesha Uwepo Wa—Wake. Hakika basi hakutakuwa na udhuru kwamba hiyo hisi ya sita haitafanya kazi.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

148 Baba yetu, wa Mbinguni, hisi ya sita, shuhuda hizi kutoka katika Biblia kwamba hisi ya sita, kama ninavyoiita imani, nilikuwa nikisoma katika Waebrania 11 juu ya hisi ya sita, imani ikiwa ni hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo ambayo hisi za dunia hazitangazi. Nasi tunaona kupitia hapo, jinsi walivyozitiisha falme, na kufunga vinywa vya simba, na kukwepa makali ya upanga. Na—naye Henoko alihamishwa Mbinguni kwa hiyo hisi ya sita.

149 Ibrahimu alikaa katika nchi ya kigeni na akapata mwana baada ya kuwa na umri wa miaka mia moja: hisi ya sita. Tumbo la uzazi la Sara lilipokuwa limekufa, hakuyafikiria mambo hayo, hakusitasita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu akimpa Mungu utukufu. Alijua Mungu alifanya ahadi na Mungu, alikuwa ameshawishika kabisa, angetimiza kile alichokuwa ameahidi.

150 Ee Mungu, nasi tunapaswa kuwa watoto wa Ibrahimu. Jinsi tulivyo kisingizio duni! Ee Mungu, iamshe hisi ya sita katika kanisa hili, miongoni mwa watu hawa usiku wa leo. Tunapoona ya kwamba ulimpa Ibrahimu hiyo ishara kuu, hapo kile kilichotukia, Mungu, ninaomba ya kwamba watamwona Malaika wa Uwepo wa Bwana usiku wa leo, nao watategemea, sio hisia zao, macho yao, bali Neno la Mungu lililotoa ahadi, na kila mtu humu ndani ataponywa, na kila mtu ambaye hajaokoka ataokolewa, na wote wasio na Roho Mtakatifu watampokea. Nisikie, Baba, ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

151 Mko tayari kupokea uponyaji wenu? Ninyi nyote? U—utaiweka hisi yako ya sita kazini? Hisi ya sita ni nini sasa? Ni imani. Nayo imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yanayoifanya Missouri kuwa mbaya: “Ninatoka Missouri, inakubidi kunionyesha,” mwajua, “sina budi kuliona.”

152 Imani ni kitu kile kinachozitiisha falme, kinacholeta haki, kinachofanya kila namna ya miujiza na ishara za hisi hiyo ya sita. Iamshe, ondoa bendeji kwenye macho yako ya kiroho, angalia kote, uone kama huwezi kuona ya kwamba Mungu angali anabaki Mungu.

153 Vema, ninyi nyote mlio na kadi za maombi pangeni mstari hapa mkono wangu wa kulia, kulingana na idadi yenu. Kadi ya maombi moja, mbili, tatu, nne, simameni. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, njoni tu moja kwa moja huku sasa upande huu. [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam. Uh-huh. Hilo ni sawa. Lete ninii. . .yako. . .Kusudi watu waweze kuzunguka, hilo ni sawa, washushe moja kwa moja humu ndani tafadhalini. Vema. Tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

154 Kundi la watu wa kidini, watu waliochaguliwa ambao kizazi chao chote, Wayahudi, ambao walikuwa wamefundishwa juu ya Masihi ajaye na yale angefanya wakati atakapokuja, na wakati alipokuja walishindwa kumtambua. Hilo ni jambo la kusikitisha, sivyo? Nafikiri hiyo ni moja ya hadithi za kuhuzunisha sana ulimwenguni. "Ulimwengu uliumbwa Naye, wala ulimwengu haukumtambua. Alikuja kwa walio Wake, walio Wake hawakumpokea." Hilo bila shaka ni wazo la kuhuzunisha.

155 Sasa angalia, walikuwa wakimtazamia Masihi. Hiyo ni kweli? Naye Masihi, wakati alipokuja, alikuwa awe Mungu-Nabii. Ni wangapi wanaojua hilo? Alikuwa afanye ishara ya nabii, kwa sababu Musa alisema angekuwa Nabii, wakati alipodhihirishwa katika mwili, angekuwa ni Nabii, afanye ishara ya nabii.

156 Hiyo ni kama tu Wayahudi sasa. Ninangojea. Mimi na Ndugu Joseph tulikuwa tukizungumza alasiri ya leo. Ndugu. . . Stockholm, Uswidi, Ndugu Lewi Pethrus alituma karibu Biblia nusu milioni. Wakati Ndugu Arganbright aliponionyesha ile picha, *Usiku Wa Manane Kasoro Dakika Tatu*. . .Hao Wayahudi wakija kutoka kote ulimwenguni, kutoka huko chini Iran, na kadhalika, hawakusikia kamwe juu ya Jina la Yesu, wamekuwa huko chini tangu ule utumwa wa Kirumi, kamwe hawakusikia kitu kama Yesu Kristo. Naye Ndugu Pethrus akawatumia Biblia hizi, walikuwa wakizisoma.

157 Na kwa hiyo, walifanya mahojiano nao. Moja kwa moja kwenye. . .Nilipata hiyo picha mwenyewe. Nao walikuwa wakiiangalia. Nao wakasema, "Kwa nini mnakuja kwenye nchi ya uenyeji wenu? Mpate kufa?" Wakiwabeba wazee mgongoni mwao, na kadhalika.

Kasema, "Tumekuja kumwona Masihi." Naam, bwana.

158 Wakati mtini unapoanza kuchipusha majani yake, majira ya joto yamekaribia. Hiyo nyota yenye ncha sita ya Daudi sasa ni taifa, bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni inapepea tena kwa mara ya kwanza kwa muda wa miaka elfu mbili mia tano. Hiyo ni kweli. Yerusalemu ina pesa zake yenyewe, sarafu zake

yenyewe, sheria zake yenyewe, serikali yake yenyewe, ni taifa tena. Yesu alisema wakati huo mtini utakapoanza kuchipusha majani yake, wakati umekaribia hata mlangoni.

159 Walipopata hii, Biblia hizi. . .Hawakuwa kama wengi wa Wayahudi wetu wa Wall Street, walikuwa huko chini wakiamini. Walipokuja kuwachukua kwa ndege, mbona, hata hawangeingia kwenye ndege hiyo, waliiogopa, kamwe hawajawahi kuona chochote. . .TWA. Mliliona katika gazeti la *Look*. Maskini rabi alikuja huko nje, na kusema, "Kumbukeni, tulipoitwa kuja kwenye nchi ya uenyeji wetu, nabii alitwambia ya kwamba tutabebwa juu ya mbawa za tai." Haleluya! Sikilizeni, "Turudishwe tukibebwa juu ya mbawa za tai."

160 Nao hao hapo kwenye nchi ya uenyeji wao, hao hapo walikuwa wakirudi tena. Wakachukua Biblia hii ndogo, nao wakaanza kuisoma, Agano Jipya. Myahudi husoma kuanzia nyuma kwenda mbele, mwajua. Basi walipomaliza kuisoma, walisema, "Ikiwa huyu Yesu ndiye Masihi," kuwaonyesha mahali walipo siku hizi, "ikiwa Yesu huyu ndiye Masihi, basi Yeye atakuwa ni Nabii. Kama amefufuka katika wafu, hebu na tumwone akifanya ishara ya nabii, nasi tutamwamini." Amina. Loo, jamani! Sawa tu!

161 Ninyi Mataifa afadhali mwinamishe nyuso zenu, saa imekaribia ambapo Mungu ataelekeza neema Yake kwa Wayahudi, nanyi Mataifa mtatiwa muhuri bila Mungu, bila rehema, mwe si kitu ila chakula cha mizinga. Kwa hiyo jipatanisheni na Mungu sasa wakati mkiwa na nafasi ya kujipatanisha na Mungu, jipatanisheni na Mungu sasa.

162 Angalieni, Yesu alipowajia Wayahudi, Yeye alifanya ishara hiyo ya Masihi, akawaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Nabii, nao wakamwita mpiga ramli, Beelzebuli, ibilisi.

163 Na ndipo Yeye. . .Kulikuwa na watu wengine zaidi waliokuwa wakimtazamia Masihi. Ni wangapi wanaojua kuna vizazi vitatu tu vya watu duniani? Kulingana na Biblia: Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Wote walikuja, wana wa Nuhu. Hiyo ni kweli. Vema. Hao ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria, ambaye ni nusu Myahudi na Mmataifa. Nao hawa Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi kuja.

164 Yesu alipanda langoni, akaketi chini pale, ndipo mwanamke mmoja akatokea, Naye akasema, "Nipe maji ninywe."

Akasema, "Si kawaida kwenu Wayahudi, hatuna uhusiano kama huo sisi kwa sisi."

165 Akasema, "Lakini kama unajua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe." Mazungumzo yakaendelea, mpaka hatimaye Yeye akasema, "Nenda, kamwite mumeo, mje hapa."

Akasema, "Sina mume yeyote."

Akasema, “Umesema vema, kwa kuwa umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

166 Akasema, “Bwana,” huyo kahaba alijua zaidi juu ya Mungu kuliko theluthi mbili ya wahubiri Marekani, hiyo ni kweli, akasema, “Bwana, naona ya kwamba Wewe ni Nabii. Sisi, sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atafanya ishara hizo, Yeye atatuambia mambo yote, lakini u Nani Wewe?”

Yesu akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

167 Ndipo akakimbia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Mlilipata? “Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Vema.

168 Sasa, Yeye alifanya ishara hiyo mbele ya Wayahudi, aliifanya mbele ya Wasamaria, bali si Mataifa. Tulikuwa Waanglo-Saxon, tulikuwa na rungu mgongoni mwetu, nasi tulikuwa tukiabudu sanamu, Warumi, na kadhalika; kamwe hakuwafanyia ishara hiyo. Naye alisema ya kwamba hicho. . .kizazi kiovu na cha zinaa, katika siku hizi za mwisho wangepata ile ishara ya Yona, ishara ya ufufuo.

169 Sasa, naye Yesu pia aliwaambia, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Sodoma ilipata ishara ya namna gani? Jambo lile lile, yule Malaika huku amegeuza mgongo wake. (Hivi umeninii. . .? Wote—watu wako wote wako, Billy? Kila mtu? Vema.) Akasema. . .

170 Ni wangapi hapa sasa ambao hawana kadi ya maombi, nanyi mnataka Mungu awaponye, inueni mikono yenu? Useme, “Na—nataka Mungu aniponye.” Sasa, kama kuna kadi zingine za maombi, walio na kadi, ingieni mstarini. Sasa, kama sivyo, mbona wewe, tutakushika, kwa vyovyote vile. Huninii. . . wewe si. . .ninataka uone. . .Laiti ungeweza tu kuchukua yale niliyosema usiku wa leo, hiyo hisi ya sita! Amini kwa moyo wako wote.

171 Sasa, wengi wenu mnatuma leso hizi huku, ninaziombea kila moja, nikijaribu niwezavyo kuzifikia. Sasa, kama nikiwakosa, niandikieni tu huko Jeffersonville, Indiana, nitawatumia moja. Unaona? Nitakutumia kwa barua. Ukiikosa, ama ukiikosa leso yako kwa njia fulani, ikipotea, niandikie tu, haikugharimu hata senti moja. Andika tu nasi. . .Bila shaka wakati mwingine watu wengine hutuma pesa kidogo, maana tunatumia mamia ya dola kwa juma kununua stempu na kadhalika, kutuma hizi, leso kote ulimwenguni pamoja na kila namna ya miujiza, na kadhalika, za ishara zikirudi kutoka kwao, maana zinawafikia wengi kuliko ninaoweza kufikia.

172 Lakini sasa angalieni, nadhani ya kwamba asilimia tisini na tano ya watu. . .Ninajua nina baadhi ya watu hapa kutoka Jeffersonville, lakini sioni yeyote wao kwenye mstari wa

maombi. Na kama walikuwako, ningewaomba vizuri watoke nje, hiyo ni kweli, kwa sababu ninaweza kuwaona huko chini nyumbani. Hii ni kwa ajili ya watu walio huku juu, watu ambao hawawezi kuingia wakati mwingine wowote.

173 Sasa, huyu hapa mama amesimama, kama ningeweza kumponya mwanamke huyo, ningekuwa la—laghai kama sikumponya, kama ningeweza kufanya hivyo, nisingestahili kusimama nyuma ya mimbara hii, Ndugu Sullivan, kama ningeweza kumponya. Lakini siwezi kumponya, tayari ameponywa kama ni mgonjwa. Sijui kwamba yeye ni mgonjwa, lakini kama ni mgonjwa, Yesu alimponya wakati alipokufa pale Kalvari, alifanya upatanisho kwa ajili yake, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Hiyo ni kweli?

174 Sasa, watu hawa waliosukumiwa hapa juu kwenye viti vya magurudumu, ninawatakeni mtazame, ninaamini jana usiku mwanamke kwenye kiti cha magurudumu, ama kitanda cha wagonjwa, ama *chochote kile*, Roho Mtakatifu alimwita, akamwondosha humo. Sasa, mara nyingi ninyi mlio kwenye viti vya magurudumu, mnaanza kusema, "Loo, ugonjwa wangu hauna matumaini." Mradi tu unaamini hivyo, hisi yako ya sita imekufa. Hisi yako ya sita, kama iko hai usiku wa leo, hii ndiyo saa ya mwisho ya mateso yako, utatoka humo, uende nyumbani, uwe mzima.

175 Mwanamume na mwanamke wamesimama hapa, ndugu na dada weusi pamoja na mvulana wao mdogo. Mnaamini usiku wa leo? Una imani, ndugu yangu, una imani, dada. Maskini jamaa huyo ni mdogo sana kujua imani ni nini, unaamini ya kwamba Mungu atamponya mtoto wako.

176 Huyu mama aliyesimama hapa pamoja na mvulana huyu mdogo hapa, wewe kuwa na imani.

177 Ninyi nyote mnaosimama karibu na viti hivi vya magurudumu, ninawatakeni mwe na imani kwa ajili ya watu hao.

178 Nanyi huko nje, baadhi yenu mlio na ugonjwa wa moyo, mtakufa katika siku chache, kansa, jambo fulani lisipofanywa mtakufa. Watu hawa wanaweza kuishi maisha ya kawaida hapa, vilema, lakini usipomshikilia Mungu, mara moja utakufa. Naam bwana. Lakini mshike Mungu, na kusema, "Mungu, ninatumia hisi yangu ya sita, naamini. Nami ninaamini ya kwamba Wewe utaniponya." Na ndipo Mungu atafanya hivyo. Hivi huamini hilo? Naliamini kwa moyo wangu wote.

179 Sasa, sitatumia njia ya upambanuzi, nisingeweza kupitisha hao hamsini hapa, nisingeweza kufanya hivyo, bali nitaomba. Sasa, kama Mungu angali anabaki Mungu, kama Mungu angali ni Mungu, basi Yeye anaweza kufanya mambo yote jinsi tu Yeye . . .

180 Hali ya juu zaidi ya—ya imani ni ipi? Kulikuwa na ya Kirumi. . .Myahudi mmoja alisema, "Njoo, weka mikono Yako juu ya binti yangu, atapona."

181 Yule Mrumi akasema, "Mimi sistahili, sema tu Neno." Hivyo ndivyo Mataifa wanavyopaswa kufanya.

182 Katika mikutano ng'ambo ya bahari, mahali mbalimbali, wanaweza kuona jambo moja la kimbinguni likitukia, kusanyiko lote litaondoka tu kwa imani. Mnaona? Wataliamini. Lakini hapa ni vigumu sana.

183 Sasa, ninyi ni Wapentekoste, huenda ninyi ni Methodisti, lakini endapo una Roho Mtakatifu wewe ni Mpentekoste, sasa, kama una hiyo hisi ya sita iliyo tayari kufanywa hai, hebu tuifanye.

184 Sasa, mwanamke huyu hapa, kwa *huyu*, kwa vyovyote vile, si—simjui huyu mwanamke. Nadhani hatufahamiani. Sasa, hapa, huyu hapa mwanamke, sijawahi kumwona maishani mwangu. Alisema hanijui nami simjui. Vema, ningejuaje, wakati aliposhuka tu, akazichanganya kadi hizi, na kumpa mtu fulani kadi, naye akaichukua, naye huyu hapa? Inatokea kwamba yeye ndiye wa kwanza jukwaani.

185 Na kama baadhi yenu nyote wakati ule ule ninapozungumza naye, aminini huko nje, muone kama Yeye hataenda moja kwa moja huko nje, na kuwapata, pia, vivyo hivyo tu. Mnaona? Sasa, kama jambo hilo linaweza kufanywa mara moja kwa mtu, labda kamwe hajawahi kuwa mkutanoni, hilo ni thibitisho kwamba ni kweli.

186 Mungu alimwambia Musa, "Chukua karama hii ushuke uende kule na kuonyesha jinsi mkono wako umeponywa ukoma." Alifanya hivyo wakati mmoja, nao Israeli wote wakamfuata hadi kwenye nchi ya ahadi. Mnaona? Hakusema kila wakati alipokutana na Mwisraeli, "Angalia hapa kwenye mkono wangu, ukoma. Unaona? Umepona." La, la. Alifanya hivyo wakati mmoja, wote wakaamini. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya: kuliona, kuliamini.

187 Sasa, hii *hapa* mikono yangu. Nijuavyo mimi sijawahi kumwona mwanamke huyu maishani mwangu, kama nilimwona, sikumjua, yeye ni mgeni kabisa. Lakini kama Roho Mtakatifu anaweza kunijia na kuniambia amesimama hapa kwa sababu gani, ama jambo fulani ambalo amefanya, ama jambo fulani analopanga kufanya, ama labda jambo ambalo—ambalo anajua kwamba sijui lolote kulihusu, hilo lingekuwa ni thibitisho ya kwamba Yeye angali ni Yesu yeye yule aliyezungumza na yule mwanamke kisimani. Hiyo ingekuwa ikithibitishia kizazi hiki cha Mataifa ya kwamba Masihi yule, Ambaye wakati mmoja aliishi katika Nguzo ya Moto katika Ubaba, akaishi katika Mwili wa kibinadamu unaoitwa Mwana

katika Uwana, na sasa katika Roho Mtakatifu ndani yako na mimi, kupitia utakaso kupitia Damu anaishi miilini mwetu.

188 Roho Mtakatifu akiishi ndani yetu: "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya. Amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda." Mnaamini hilo?

189 Sasa, ninataka kuwaulizeni kwenye viti vya magurudumu. Sasa, kama ningeweza kumponya mwanamke huyu, ningemponya; kama ningeweza kukuponya, ningekuponya, siwezi. Lakini kama Bwana Mungu, kwa kuwa yuko karibu nami, kama Bwana Mungu ataniambia jambo fulani kumhusu mwanamke huyo, na awe ndiye hakimu kama ni kweli ama si kweli, kwamba yeye anajua ya kwamba sijui, mnajua ya kwamba haina budi kuhitaji namna fulani ya nguvu za kimbinguni hapa kufanya hivyo. Hiyo ni kweli?

190 Utaamini kuwa ni Mwana wa Mungu kulingana na ahadi Yake, kwamba Yeye aliahidi angefanya hivyo? Je, mtaamini ninyi nyote kupitia hapa? Ukubali uponyaji wako basi na kuamini kwa moyo wako wote? Kisa kimoja tu kingalitatua hilo kama kweli mngemaanisha hilo. Amina. Hiyo ni kweli kabisa. Laiti mngaliamini jambo hilo moja! Bila shaka ingekuwa ni kweli.

191 Vema, mama, sasa, nitasimama tu hapa kwenye maikrofoni hii, maana wakati maono yanapokuja sijui jinsi nilivyo, ninavyozungumza kwa sauti ya chini, ama ninavyozungumza kwa sauti kubwa. Lakini nina kusanyiko hili hapa likiahidi ya kwamba watapokea uponyaji wao kama Roho Mtakatifu atanifunulia jambo fulani kukuhusu wewe ambalo mimi, unajua kwamba silijui. Sasa, hilo litakuwa. . .Je, linge—lingekutia moyo, na kukufanya uamini kama Yeye angefanya hivyo, pia? Lingekutia moyo? Hakika lingefanya hivyo.

192 Sasa, sasa, ninazungumza tu nawe kama tu vile Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani. Unaona, Yeye alimshika kwanza, maana alikuwa ndiye wa kwanza, unaona, hivyo ndivyo inanibidi kufanya, pia, kupata. . .Unaona, wewe ni mwanadamu, una roho, unayo nafsi; mimi ni mwanadamu, nina roho na nafsi. Ninajua sasa kwamba wewe ni Mkristo, kwa sababu roho yako imeanza kunishuhudia ya kwamba wewe ni Mkristo. Hiyo ni kweli. Unaona? Inajisikia kukaribishwa, kama sivyo, ingekuwa inasukumia mbali.

193 Uliwahi kuwa katika mmoja wa mikutano hii na kuona mambo haya yakifanywa? Umeyaona yakifanywa. Umewahi kuona wakati wenye dhambi wanapokuja, na kadhalika, ukaona jinsi inavyosukuma kutoka kwao namna hiyo? Itaninii tu, *sasa hivi*, itawaambia, "Wewe ni mwenye dhambi. Unafanya *hivi-na-vile*. Unafanya *hivi-na-vile*." Unaona?

194 Sasa, kama ukiamini kwa moyo wako wote, na yote yaliyo ndani yako, Mungu ataweza kuniambia shida yako

ni nini, ama kitu fulani kuihusu, kisha utaupokea, na hilo litawafanya wote waamini. Watu hawa waliolemaa walisema wangeamini, wagonjwa, ugonjwa wa moyo, na kadhalika, walisema wangeamini. Kwa hiyo basi kila mtu aamini, na mstari wote ungeliamini huko chini, hakutakuwa na haja ya kuupitisha mstari wa maombi, kila mtu kweli anataka kutumia hiyo hisi ya sita, na kuendelea tu, aseme, “Asante Bwana, Yeye huniponya.”

195 Huo ndio msimamo Wake kwa kila mmoja wao, imetokea tu kwamba wewe ndiwe mtu ambaye ameletwa hapa juu, kuna wengi, wengi zaidi kote kote huko. Labda huenda Roho Mtakatifu baada ya kitambo kidogo akalipitia kusanyiko lote, sijui atakalofanya. Ndipo ninapokuwa dhaifu sana, mwanangu, ama baadhi yao pale, Gene, ama baadhi yao, watakuja waniguse ubavuni, ninajua ni . . . Sina budi kuondoka basi, mnaona, maana sininii . . . Hujui mahali ulipo wakati mwingine, baada ya maono mengi sana inaonekana kana kwamba kila kitu ni ono basi, mnaona. Yesu alisema, “Nyingi kuliko hizi mtafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu,” mambo aliyokuwa ameyaona.

196 Sasa, ninaona shida ya huyu mwanamke, amekuja hapa kwa ajili ya maombi, na maombi ni kwa ajili ya kivimbe kidogo, nacho hicho kivimbe kiko kwenye mkono. Hiyo ni kweli, sivyo.

Sasa unaamini?

197 Sasa, hicho kivimbe kimefichwa kwangu, lakini si kwa Mungu. Nikwambie kiko kwenye mkono gani? Wa kulia. Hiyo ni . . . Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli.

198 Sasa, unaamini kwa moyo wako wote? Sasa, je, hiyo hisi ya sita inakufanyia jambo fulani? Je, umepofushwa tu? Na kusema, “Vema, hilo ni zuri sana.” Unaona? Ama kweli hiyo hisi ya sita inaanza kufanya kazi? Sema, “Mungu asifiwe! Ninajua ya kwamba mtu huyo hamjui mwanamke huyo. Sasa, Yesu Kristo pekee ndiye angemjua, Naye aliahidi atafanya hivyo.” Hiyo inamaanisha ya kwamba utakuwa mzima basi kama unaweza kuliamini.

Unasema, “Labda ulibahatisha alichokuwa nacho.”

Nisingeweza kubahatisha hilo, hakuna kubahatisha kwa hilo.

199 Labda nitakwambia jambo lingine. Wewe hutoki hapa, unatoka Lima. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi White, Bibi White. Hiyo ni kweli. Mungu atakuponya sasa, nenda nyumbani na uamini kwa moyo wako wote.

200 Sasa, unaamini? Kila mmoja wenu? Mwaminini Mungu. Kama unaweza kuamini, “Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio. Kama unaweza kuamini!”

201 Vipi kama ningekwambia, uliponywa ukiketi kitini, ungeniamini? Nenda zako tu basi, maana uliponywa. Mwamini Mungu.

202 Sasa, vipi kama nikiweka mikono yangu juu yako, na kusema, "Shetani, toka kwa mvulana huyu," ungeamini? Ungepona? Njoo hapa.

Shetani, mwache mvulana huyu, katika Jina la Yesu! Amina.

Nenda ukiamini sasa. Amini.

203 Vipi kama ningeweka mikono juu yako, na kusema, "Shetani, toka kwake," ungeamini?

Shetani, toka kwake, katika Jina la Yesu! Amina.

Mungu akubariki, nenda ukaamini.

204 Kama ningekwambia shida yako, ingekusaidia, ama ungependa nikuwekee tu mikono? [Ndugu huyo anasema, "Naam, ingenisaidia."—Mh.] Ni gani ingekusaidia, mimi kukwambia shida yako ni nini? Iko mgongoni mwako. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Basi nenda nyumbani, ukaponywe, katika Jina la Yesu. Vema.

Unaamini kama nikikwambia tu jambo fulani, nikuwekee mikono, lingekuponya? Njoo hapa basi.

Katika Jina la Yesu, jalia aponywe. Amina.

Amini. Vema.

205 Na wewe je? Ninaamini ninakujua. Hiyo ni kweli. Nitakuwekea tu mikono, na kusema:

206 Shetani, mwache ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo! Amina.

207 Amini sasa, ndugu, nenda kwa moyo wako wote.

208 Mnaamini ninyi nyote? Vema, sikilizeni, haya ndiyo nisiyoweza kupata. Mnaona? Ni kwa nini wakati Roho Mtakatifu atakuja na kufunua mambo hayo . . .? Yeye ananiambia shida zote za watu hao kama ningesimama kwa dakika moja, lakini basi hao wengine wasingeingia mstarini. Si ni jambo zuri sana kumwona Bwana, wakati watu wanapopita wawe na imani ya kutosha kuponywa, wawekewe mikono, kadiri ingekuwa ku—kuwa na upambanuzi mkiisha kuona jambo hilo likifanywa? Hivi tumekuwa Wamarekani hivi kwamba inatubidi kutumbuizwa na Roho Mtakatifu?

209 Hapa, njoo hapa. Sikujui. Lakini hatufahamiani. Hiyo ni kweli? [Ndugu huyo anasema, "Ninakujua."—Mh.] Unanijua, lakini mimi sikujui, bali Mungu anatujua sote wawili. Kama Mungu ataniambia shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Kwa moyo wako wote? Vema. Ugonjwa wa moyo, hiyo ni kweli kabisa. Unaamini sasa kwa moyo wako wote? Unaamini utapona? Mmetoka mbali sana kwa ajili ya jambo hili, sivyo? Kote kote kutoka California. Hiyo ni kweli.

210 Umemleta mkeo, pia? Anataka uponyaji, pia. Hakupata kadi. Lakini ana shida kwenye nyonga yake, ilisababishwa na kuanguka. Hiyo si ni kweli? Nendeni nyumbani, mtapata afya nyote wawili. Nendeni mkaamini.

211 Sasa, sasa, hiyo ni sawa tu na . . . Mnaona?

212 "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana."

213 Unaamini, dada? Nikikuwekea tu mikono, unaamini ungepona? Njoo basi.

Katika Jina la Bwana Yesu, mponye mwanamke huyu.

Vema. Njoo mama.

214 Sasa mnaona? Sasa, kwa nini? Mwanamke huyo ameponywa tu kama yule mwanamume mwingine. Kwa nini hatuwezi kusema, "Bwana asifiwe," kwa kumponya mwanamke huyo? Mnaona?

215 Hapa, sasa, unajua ninajua shida yako. Unajua hilo kadiri tu nijuavyo mimi, unajua ya kwamba Mungu angeweza kuniambia. Sasa, kama ningekwambia ingekusaidia? Mishipa yako ndiyo inayofifia. Hiyo ni kweli kabisa. Amini kwa moyo wako wote, nenda ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Amini.

Unaamini, dada, kwa moyo wako wote?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

Unaamini kwa moyo wako wote dada?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe. Amini.

Njoo, dada. Unaamini kwa moyo wako wote?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

Sasa, hivyo ndivyo hasa Mungu alivyosema lifanywe. Hiyo si ni kweli? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe. Amina.

Unaamini kwa ajili yake?

Katika Jina la Yesu Kristo ibilisi na amwache mtoto huyu. Amina.

Nenda sasa, ukaponywe.

216 Unataka kula chakula chako cha jioni, uondokee ugonjwa huo wa tumbo? Nenda ukale chakula chako cha jioni upate afya, katika Jina la Yesu.

217 Unaamini kwa moyo wako wote? Unaona? Endelea kwenye . . . Chukua hiyo hisi ya sita, uondoe hizo tano za kale njiani, amini.

218 U hali gani? Kama ningekwambia ndiyo au la, ungeamini, kwa vyovyote vile, huh? Ungeamini, kwa vyovyote vile. Vema. Kivimbe hicho kidogo kwenye mgongo wako, kilicho katikati ya mabega yako, nenda ukiamini na upate afya. Unaamini? . . . ? . . . Amina. Amini.

Njoo, ndugu. Unaamini?

Katika Jina la Yesu, jalia aponywe.

Njoo. Unaamini ndugu?

Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono yangu juu yako, utapona. Amina.

Amini sasa.

Unaamini, bwana?

Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe. Amina.

Yesu anakufanyia kama ukiamini.

Katika Jina la Yesu Kristo uponywe.

Hiyo ndiyo njia, ndugu. Jambo ndilo hilo. Hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo.

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe. Amina.

219 Njoo, dada. Kama upako wa Roho Mtakatifu upo hapa kufanya miujiza kama hiyo, hakika ungeamini nilitiwa mafuta Naye, sivyo?

Basi katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe. Amina.

Unaamini, ndugu?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

220 "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana."

Huyu ndiye mgonjwa anayefuata? Vema.

221 Unaamini, dada, kwa moyo wako wote? Jambo ndilo hilo. Amina. Kweli aliipata. Niliangalia tu, alikuwa na kivuli juu yake, na wakati kilipoondoka nilishangaa kilipatwa na nini, kikageuka, sasa kimetoweka kwa sababu aliamini. Mnaona? Jambo ndilo hilo.

222 Sikujui, hunijui mimi, hatufahamiani. Lakini Mungu anakujua, Naye anajua niko hapa kukusaidia nikiweza. Unaamini hilo?

223 Hebu kidogo, jambo fulani lilitukia kwenye kusanyiko, mahali fulani, mahali fulani. Jambo ndilo hilo, anzeni kuamini huko nje. Vema, shida yako iko mgongoni mwako, hiyo ni kweli, una shida ya mgongo. Bibi Finnhoeffer, nenda nyumbani ukapate afya, katika Jina la Bwana Yesu, uwe mzima.

Njoo, ukiamini kwa moyo wako wote. Unaamini, bwana?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

224 Njoo. Sasa, kama ningekwambia shida, ama sikukwambia, ama chochote kile, ungeamini, kwa vyovyote vile? Basi ninii yako ya kike. . . ugonjwa wa kike tayari umekuacha, endelea. Naam, nililisema, kwa vyovyote vile. . .?. . . Hiyo ni kweli.

225 Vema. Unaamini ya kwamba Mungu ataponya wasiwasi wako? Vema. Endelea, uwe mzima, katika Jina la Yesu. Amini kwa moyo wako wote.

226 Unataka kuondokana na ugonjwa huo wa tumbo? Vema. Nenda ukale chakula chako cha jioni, upate afya, katika Jina la Bwana. . .

Unaamini kwa moyo wako wote? Vema.

Unaamini, dada?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

227 Vema. Unaamini kwamba mvulana huyu mdogo anaweza kuondokana na shida hii?

228 Namlaani ibilisi aliyemfanyia hivi mtoto huyu! Jalia aponywe, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

229 Mchukue sasa, usiwe na shaka. Angalia kitakachompata kama unaweza kuamini.

Unaamini kwa moyo wako wote?

Katika Jina la Yesu Kristo na uponywe.

230 Kuna uponyaji unaoendelea kuja kutoka hapa. Ni maskini mwanamke huyo aliyeketi huko nyuma amevaa kofia ya kahawia, kidogo ni mwembamba, anaugua TB. Vema, dada. Sikujui, na wewe hujui. . .Naam, unapaswa kunijua mimi, uliponywa wakati mmoja katika mkutano wangu, ninaiona, ilikuwa huko Fort Wayne, Indiana. Haleluya! Jambo ndilo hilo. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako, ulikuwa na shida gani hapo? Ulikuwa na uvimbe, naye Mungu akakuponya huo, BWANA ASEMA HIVI. Haleluya!

231 Ninakupa changamoto kuamini! Kuna wengi sana wanaoamini. Mwaminini Mungu.

Unaamini, dada?

Katika Jina la Yesu, nenda ukaponywe, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Unaamini, ndugu?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

Unaamini, ndugu?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

Unaamini, dada?

Katika Jina la Yesu, nenda ukaponywe.

Unaamini, ndugu?

Katika Jina la Yesu, nenda ukaponywe.

232 Unaamini kwa ajili ya huyo mtoto mchanga? Sasa, angalia, ninajua ni shida ya uzazi, lakini hiyo haina uhusiano wowote. . . Kile ibilisi alichofanya wakati wowote, Mungu anaweza kukiondoa. Unaamini hilo?

233 Namlaani ibilisi aliyemfanyia mtoto huyu hivi! Katika Jina la Yesu Kristo, mtoto huyu na awe mzima. Amina.

Unaamini, dada?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

Unaamini, dada?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukawe mzima.

Unaamini, dada?

Katika Jina la Yesu, nenda ukaponywe.

234 Unaamini, dada? (Je, huo ndio mwisho wa mstari wa maombi?) Vema, nitazameni hapa kwa dakika moja tu. Unaamini kwa moyo wako wote? Kama Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini, unaamini? Jambo moja, macho yako yanaharibika. Hiyo ni kweli. Hilo silo jambo muhimu, una uvimbe, uvimbe uko tumboni. Wewe hutoki hapa, rudi Illinois ukapate afya, Yesu Kristo alikuponya.

235 "Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana." Unaamini hilo?

236 Mtu huyo aliyeketi moja kwa moja huko nyuma, ana, amemleta mtoto mchanga, ana tundu moyoni mwake. Unatoka Chattanooga, Tennessee. Bw. Kirkline, nenda nyumbani na uamini, moyo wa mtoto huyo utapona. Yesu Kristo anauponya. Haleluya!

237 Hizo ndizo nguvu za Mungu wetu. Mwaminini Mungu.

238 Mwanamke mwingine, aliyeketi hapo kutoka Memphis, Tennessee, huku juu, akimwombea binti aliyepotea, mwamini Mungu.

239 Ninamtafuta mwanamke, siwezi kumwona kwenye kusanyiko, lakini yuko hapa, mahali fulani, anaomba. Mungu anisaidie kumpata. Mtu fulani mwenye imani, ana ugonjwa wa moyo na kisukari. Jina lake ni Bibi Wells. Mwamini Mungu. Mahali fulani, siwezi . . . [Dada mmoja anasema, "Huyu hapa."—Mh.] Vema, vema, dada, imani yako imekuokoa.

240 Isitoshe, ugonjwa wa moyo hutembea katika familia yenu. Huna kadi ya maombi, sivyo? Kwa sababu ninyi . . . La, maana kadi zote za maombi ziko juu. Ugonjwa wa moyo unatembea katika familia yenu, una ndugu aliye na ugonjwa wa moyo. Ndugu huyo hayupo hapa, ndugu huyo anaishi Baltimore, Maryland. Naye pia hajaokoka, kwa sababu ametiwa uvuli wa kivuli cheusi, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

241 Unaamini kwa moyo wako wote? Hiyo hisi ya sita itafanya kazi juu yako? Wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi papa hapa.

242 Ee Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, mtume Roho Wako Mtakatifu wakati huu na kumponya kila mtu katika Uwepo wa Kiungu, kupitia Jina la Yesu Kristo.

243 Mnaliamini? Ni wangapi hapa ndani mnaotaka kumjua Yesu kama Mwokozi wenu? Simameni kwa miguu yenu. Mko karibu na Yeye. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni sawa. Ajabu!

244 Ni wangapi wanaomtaka Roho Mtakatifu? Simameni kwa miguu yenu. Unayetaka ubatizo wa Roho Mtakatifu, simameni kwa miguu yenu, kila mmoja wenu. Ni wengi sana hapa nje siwezi kuwafikia sasa, pangeni mstari moja kwa moja kwenye chumba hiki, ili tuweze kukutana nanyi *hapa*.

245 Katika Jina la Yesu kama utakuja kwa uaminifu, utajazwa na Roho Mtakatifu, uokolewe na dhambi zako zote. Ingia chumbani usiku wa leo, huu ndio wakati, sogea upande *huu* uingie chumbani. Wote waliopo hapa wanaomwamini Mungu, wanaotaka kuokolewa na kujazwa na Roho Mtakatifu, songeeni moja kwa moja mwingie kwenye chumba hiki, ili tuweze kuwahudumia.

246 Kama kuna mtu yeyote hapa kutoka kanisani mwangu huko chini Jeffersonville ambaye bado hajampokea Roho Mtakatifu (Ndugu Collins, na hao wote wamempokea Roho Mtakatifu tangu wamekuwa hapa. Loo, wameiharibu nchi.), njoni huku, huu ndio wakati wenu kuupokea, sasa hivi, ingieni. Usitoke humo mpaka utakapompokea Roho Mtakatifu.

247 Njoni sasa, enyi wenye dhambi wote. Ingieni humu ndani mkamtafute Mungu kwa ajili ya wokovu. Hiyo ndiyo njia.

248 Ninampa changamoto kila mwanamume na kila mwanamke aliye katika Uwepo wa Kiungu, ambaye ni mgonjwa, shida yoyote uliyo nayo, ninakupa changamoto kumwamini Bwana Yesu Kristo wakati nikiwaombea. Utafanya hivyo? Ni wangapi watakaoahidi watafanya hivyo? Kama Mungu anaweza kunipa nguvu hapa za kupambanua roho. . .Ninakwambia, siwezi kukuponya, tayari umeponywa, Yesu alikuponya wakati alipokufa kwa ajili yako. Hebu hiyo hisi ya sita isife ganzi, itumikishe sasa na uiamini.

249 Vipi kuhusu ninyi watu wote hapa katika viti hivi vya magurudumu, mnaamini? Basi hebu na tumwinulie Mungu mikono yetu.

250 Ee Bwana Mungu, jalia ujumbe huu usipite bure, jalia nguvu za Mungu zisiende bure hapa usiku wa leo, bali Mungu wa Mbinguni na ashushe nguvu za kusadikisha na kumponya kila mtu. Ibilisi na amwache kila mtu aliye na kansa, ugonjwa wa moyo, kilema, lukemia, aina yoyote ya ugonjwa. Ninaipa changamoto kwa karama, iliyohudumiwa na Malaika, iliyotumwa katika mateso ya Yesu Kristo kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka!

251 Toka ndani yao, Shetani! Ninakuamuru, katika Jina la Yesu Kristo, utoke ndani yao!

252 Sasa, wote wanaomkubali Kristo kama Mponyaji wao, sijali mna shida gani, haileti tofauti hata kidogo, kama unamwamini Mungu, simama na uukubali, katika Jina la Yesu Kristo. Hiyo ndiyo njia. Amina! Mungu awabariki. Jambo ndilo hilo! Hilo ni kamilifu, kamilifu.

253 Mungu awabariki. Vema, Ndugu Sullivan.

60-0611E Imani Ndiyo Hisi Ya Sita
Miami Valley Chautauqua Campgrounds
Chautauqua, Ohio Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org